epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Jumanne Julai 2, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581725
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22
UNITED WATETA NA DE LIGT

# NI TAHARUKI

UKURASA WA 5
## MBOWE AWAJIBU WANAOKIHAMA CHAMA

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amewajibu wanasiasa...



UKURASA WA 5
## WADAU WA SUKARI WATAJA MKAKATI KUONGEZA UZALISHAJI



UMOJA wa Wazalishaji Sukari Tanzania (TSPA), umesema uzalishaji wa bidhaa hiyo unaoendelea sasa unatarajia kufikia tani 528,000 hadi 663,000 mwaka...

UKURASA WA 19
## RAIS RUTO ASEMA HANA HATIA VIFO VYA WAANDAMANAJI KENYA

RAIS wa Kenya William Ruto amesema kuwa hana hatia na vifo vya waandamanaji vilivyotokea mapema wiki iliyopita katika maandamano ya...



## WHO: Watanzania milioni sita hatarini kupofuka

UKURASA 4



Rehema Mrisho ambaye ni Mama wa kijana Lilenga Lilenga aliyetekwa.
**PICHA ZOTE: ADELA MADYANE**

## • Utekaji

Kigoma washika kasi, wanaoteka hudai fedha ndugu...*Endelea ukurasa 2*






Kamanda wa Polisi mkoa wa Kigoma, Philemon Makungu



Kijana aliyetekwa, Ramadhan Shaban



## Aweso awa mbogo, aagiza vigogo DAWASA kusimamishwa kazi

UKURASA 3

**MICHEZO** NYOTA YANGA SASA KUMTESA GAMONDI UK.24

**KATUNI** UK.6

# Utekaji washika kasi Kigoma

**Na Mwandishi Wetu,**
KIGOMA

MATUKIO ya watu kutekwa kwa kutumia magari na watu wenye silaha za moto (bastola) katika Kata ya Kibirizi na maeneo mengine mkoani Kigoma, yamesababisha taharuki.

Matukio hayo yanadaiwa kushika kasi kuanzia mwezi Mei mwaka huu, huku watekaji wakidaiwa pia kutumia sindano za dawa ya usingizi.

Imedaiwa kuwa watekaji hao wanapofanikiwa kuteka hudai fedha kwa ndugu wa watu hao, huku waathirika wakishindwa kutoa ripoti na kuzua maswali.

Ramadhan Shaban (21) Kocha wa Kichwere FC, mtoto wa tano katika familia ya mzee Shaban, mkazi wa Mtaa wa Bushabani, Kata ya Kibirizi aliiambia Nipashe jinsi alivyotekwa na watu wasiojulikana waliokuwa kwenye gari jeusi.

Anasimulia kuwa akiwa anatokea kwa bibi yake kufunga taa za sola Mtaa wa Buronge, majira ya saa tatu usiku Mei 14, mwaka huu, alikutana na watu asiowafahamu.

Alipofika barabara kubwa ya lami mbele aliliona gari jeusi likiwa limeegeshwa pembezoni, kabla hajalifikia alimulikwa na taa za mwanga mkali wa gari hilo akakosa mwelekeo na kutaka kuanguka ndipo walipotokea watu watatu na kuanza kumshambulia na kumchoma sindano maeneo ya shingoni iliyomfanya kupoteza fahamu.

"Sikujua chochote kilichoendelea mpaka nilipokuja kuamka na kujikuta nipo katika chumba ambacho nilihisi nipo na watu wengine ila sikuweza kuwaona kwa kuwa nilikuwa nimefungwa na kitambaa usoni," anasema Shaban.

Baadaye alikuja mtu na kumfungua mikono na kitambaa ili atoe nywila kwenye simu yake na kuwapatia namba za baadhi ya ndugu zake na baada ya kufanya hivyo alifungwa tena na kamba na kitambaa usoni.

Hakujua kitu kingine kilichoendelea baada ya kumpa mtekaji namba za simu za wazazi na ndugu zake mpaka alipojikuta yupo Hospitali ya Rufani ya Mkoa Maweni akipatiwa matibabu na ndugu zake kumwambia alikaa kwa watekaji kwa muda wa siku 11.

Akielezea upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii anasema; "Muda wote niliokuwa huko nilijisaidia nilipokuwa nimekaa zaidi haja ndogo, sikupata haja kubwa kwakuwa nilikuwa nikilishwa pumba, unga na maji."

### NDUGU WAELEZA

Akizungumzia tukio hilo kaka yake, Bilali Shaban, anayeshughulika kubeba mizigo katika Mwalo wa Kibirizi, anasema baada ya mdogo wake kutorudi nyumbani mpaka saa tano usiku, walimtafuta kwa kumpigia simu bibi yake.

Bibi yao aliwajibu kuwa kijana huyo alishaondoka muda mrefu, ndipo walipoanza kumtafuta kwa marafiki bila mafanikio.

"Wasiwasi ulitanda, tulitoka na kuomba msaada kwa majirani ambao walitusaidia kumtafuta, tulianza kwa kutoa taarifa polisi ambao walitushauri kwenda hospitali kwa kuwa saa 24 za kufungua kesi ya kupotea kwa mtu zilikuwa bado ili kufungua jalada, tulifanya hivyo ila hakuwepo huko pia, kwakuwa usiku ulizidi kuwa mwingi tulirudi nyumbani na kusubiri kukuche ili tuendelee na kumtafuta," anasema Bilali.

Juni 15, walitoa tena taarifa ya upotevu wa ndugu yao katika kituo kikuu cha polisi na huko walisema hayupo na kuwataka waende katika kituo cha Kigoma mjini, hata hivyo, hawakufanikiwa kumpata.

"Tulimtafuta siku nzima, kila mahali, lakini hatukumpata, tulikata tamaa na kuwa na maswali mengi kichwani ambayo hayakuwa na majibu, hatukuweza kuwaza mambo mabaya juu yake kwa kuwa Ramadhan si kijana mwenye tabia za ajabu," anasema Bilali.

Aidha, anasema saa saba usiku Mei 16, alipigiwa simu na namba mpya, mara tatu, lakini hakupokea kutokana na uchovu, aliziona simu hizo alfajiri saa 10:30 aliposhituka kutoka usingizini zilizoambatana na ujumbe mfupi wa maneno uliosomeka:

"Mtu wenu mnayemtafuta tunaye sisi, na kama mnamuhitaji itabidi mfuate masharti tutakayowapatia" mnatakiwa mtupatie Sh. milioni 2.5, msipofanya hivyo ndani ya muda tuliowaambia tutamuua na kuchukua figo na maini, maelekezo ya kutuma pesa tutakupatia," ulisema ujumbe huo.

Asubuhi, Mei 17 alifika Kituo Kikuu cha Polisi akiwa na ujumbe na namba ya simu iliyompigia ikihitajika Sh. 50,000 kwa ajili ya ku "track" namba hiyo japo polisi hao hawakurudi na majibu ya uchunguzi wao kwa wahusika mpaka kupatikana kwa ndugu yao licha ya kupewa mwendelezo wa kila taarifa na vitisho walivyokuwa wakivipata kutoka kwa watekaji.

"Tulitoa pesa ya kufuatilia hiyo namba, na tuliendelea kutoa taarifa ya vitisho na taarifa nyingine kutoka kwa watekaji kwa mpelelezi wa kesi tuliyepewa na jeshi la polisi, alituambia tusichukue hatua yoyote, tuliachie jeshi la polisi, lakini kwakuwa vitisho vilikuwa vingi na muda waliotupatia wa kulipa hizo pesa ulikuwa umeisha polisi wakiwa kimya ilibidi tutafute pesa hizo ili kuzituma kupitia namba na maelekezo waliyotupatia," anaeleza Bilali.

"Ilipofika Juni 24, tarehe ambayo watekaji walisema ni siku ya mwisho, asubuhi walipiga simu na kutuambia tuandae matanga kwakuwa ikifika usiku hatujatuma fedha hiyo watamuua Ramadhan, tulikaa kama familia na kuhakikisha fedha imepatikana.

"Tulisubiri watupigie simu wao kwakuwa namba walizokuwa wanatumia kutupigia hazikuwa zikipatikana baada ya kuongea na sisi, na ilipofika usiku walipiga simu na kutupa melekezo ya kutuma hiyo pesa pamoja na ya kutolea, hivyo tulituma Sh. 2,554,000 ilikuwa ngumu sana kwetu kutokana na hali ngumu ya maisha tuliyonayo," anasema Bilali.

> **"Ilipofika Juni 24, tarehe ambayo watekaji walisema ni siku ya mwisho, asubuhi walipiga simu na kutuambia tuandae matanga kwakuwa ikifika usiku hatujatuma fedha hiyo watamuua Ramadhan, tulikaa kama familia na kuhakikisha fedha imepatikana.**

Baada ya watekaji kupokea muamala, walipewa maelekezo ya kumpata Ramdhani siku inayofuata, na saa 3:00 usiku Mei 25, mwaka huu, watekaji waliwapigia simu wakiwataka wawe na usafiri kwenda Kijiji cha Msimba eneo lilipo dampo ili wakamchukue ndugu yao, walifanya hivyo na kumkuta akiwa amefungwa kamba miguu na kitambaa machoni.

"Tulimfungua kamba na kuelekea kituo cha polisi cha central ambapo walitupatia PF3, tukampeleka Hospitali ya Rufani ya Maweni, kutokana na hali kuwa mbaya alitundikiwa dripu za chakula, ili apate nguvu pamoja na kupatiwa huduma nyingine muhimu.

"Tunamshukuru Mungu sasa anaendelea vizuri japo matendo kama haya bado yapo mengi katika jamii na hatujui chanzo chake ni nini," alisema huku akiliomba jeshi la polisi kuchukua hatua dhidi ya vitendo hivyo vinavyoendelea katika jamii.

### WENGINE WALIOTEKWA

Mkazi wa Mwandiga Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, Lilenga Lilenga (49), anayejishughulisha na shughuli za uvuvi alipotea tangu Mei 11, mwaka huu alipokuwa kwenye shughuli zake mwalo wa Kibirizi.

Akizungumza na mwandishi wa gazeti hili, mke wa Lilenga, Johari Kabwe, anasema sasa ni zaidi ya mwezi mmoja mume wake hajulikani alipo licha ya kutoa taarifa jeshi la polisi ambapo anadai hawawaambii chochote kuhusiana na maendeleo ya kutambua alipo mume wake huku akilitilia shaka jeshi hilo kuhusika na upotevu wa mume wake.

Mama mzazi wa Lilenga, Rehema Mrisho anasema zimefanyika jitihada mbalimbali za kumtafuta ikiwemo kumtangaza kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii bila mafanikio.

Aidha, anaiomba serikali kuingilia kati suala la mtoto wake kupotea ili aweze kurejeshwa, ambaye ni wa pekee anayemlea katika umri wake wa uzee.

Joyce Christant (maarufu mama Rose) mkazi wa Gungu, anakiri kupotea kwa mtoto wake wa kike (20), ambaye hakulitaja jina lake akidai hataki kuzungumza lolote kuhusu tukio hilo kwakuwa hakupata ushirikiano kutoka polisi.

Akisimulia tukio hilo alisema mtoto wake alichukuliwa majira ya saa 2:30 usiku wa Mei 14, 2024 alipokuwa akiuza bidhaa dukani ndipo walifika watu wakihitaji maji ya kunywa na alipowapelekea kwenye gari hakurudi tena.

Mama Rose anasema ili kumpata mwanawe ilibidi afuate maelezo ya watekaji na kulipa Sh.2,500,000 na kisha kurejeshewa mwanawe ambaye tayari alikuwa ameshapelekwa jijini Mwanza.

### VIONGOZI SERIKALI WANENA

Mwenyekiti wa Mtaa wa Butunga, Hamis Kalimwagu alithibitisha kuwapo kwa tukio hilo na matukio mengine ambayo yamekuwa yakiendelea kutokea katika mtaa wake yakiwamo kubomoa nyumba, kuiba mifugo na watu kuchomwa visu.

Aidha, aliyahusisha matukio hayo na kusitishwa shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika kwa miezi mitatu hali inayosababisha kuwakosesha kipato na kutumia mbinu za utapeli kama wanavyofanya.

Mwenyekiti huyo aliiomba serikali kupunguza miezi ya kufungua ziwa hilo ambalo linategemewa na wananchi hao kujipati kipato.

### POLISI

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, Philemon Makungu, amethibitisha kuwapo kwa matukio hayo na kusema wanaendelea na uchunguzi kila linaporipotiwa tukio la upotevu.

Amewataka wananchi kutotoa pesa zinazoombwa na watekaji kwa kuwa kitendo hicho kinaweza kuongeza magenge ya kihalifu na badala yake watoe taarifa katika kituo cha polisi ili hatua ziweze kuchukuliwa na watekaji waweze kutiwa mbaroni.

RPC Makungu anasema endapo wananchi watafika vituo vya polisi na kujibiwa vibaya wanapaswa kujua majina ya waliowajibu, ili hatua za kinidhamu ziweze kuchukuliwa dhidi yao kwa sababu wapo kwa ajili ya kusaidia watu na si kuumiza hisia zao.

"Mtu hawezi kuja kituo cha polisi bila sababu za msingi, akijibiwa vibaya akathibitisha muda aliofika na muonekano wa polisi aliyemjibu vibaya kisha atoe taarifa kwa kamanda wa polisi kwakuwa wanaingia kwa zamu ni rahisi kujua nani alikuwapo kwa muda huo ili tumkemee na asirudie," anasema Makungu.

Aidha, alisema upelelezi wa tukio hilo bado unaendelea.


## INVITATION FOR PROVISION OF PROJECT AUDIT SERVICES

TaTEDO Sustainable Energy Services Organization (TaTEDO -SESO) wishes to engage the services of an audit firm for the purpose of auditing the program leading the change, which is implemented in partnership with WWF Tanzania. The audit shall be carried out in accordance with international audit Standards (ISA) Issued by IAASB and International Standards on Related Services (ISRS)4400.

**Objectives and Scope of the Audit.**
The objective is to audit the financial report for the period 1/7/2023-30/6/2024 as submitted to WWF Tanzania and to express an audit opinion according to ISA, applying ISA 800/ISA 805, on whether the financial report of the program is in accordance with the cooperation partner's accounting records and WWF Tanzania requirements for financial reporting as stipulated in the agreement including appendices between WWF Tanzania and TaTEDO-SESO.

Interested applicants can obtain detailed reporting requirements and budget to carry out the audit upon request through email **energy@tatedo.or.tz.**

Only expressions of interest received within 14 days from the date of this advertisement will be considered. The audit of the program is required to be concluded before **31/8/2024.**

**Executive Director,**
**TaTEDO SESO,**
**P.O Box 32794,**
**Dar es Salaam.**

HABARI KITAIFA

# Aweso awa mbogo, aagiza vigogo DAWASA kusimamishwa kazi

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso ameiagiza Bodi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), kuwasimamisha kazi vigogo wawili wa mamlaka hiyo, akiwamo Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu, Kiula Kingu ili kupisha uchunguzi.

Mwingine ni Mkurugenzi wa Uzalishaji na Usambazaji Maji wa DAWASA, Shaban Mkwanywe.

Ameagiza mamlaka hiyo kuwa chini ya Wizara ya Maji kwa muda mpaka ufumbuzi utakapopatikana.

Alitoa agizo hilo jana kwenye ofisi za makao makuu ya DAWASA, Ubungo mkoani Dar es Salaam, baada ya kufanya ziara ya kushtukiza katika maeneo ya Chuo Kikuu cha Ardhi, Mbezi, Mshikamano na Tegeta A ambako kuna matangi ya maji.



Viongozi hao wamesimamishwa kutokana na ripoti iliyotokana na ziara ya Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mhandisi Mwajuma Waziri, iliyobaini utendaji usioridhisha ndani ya taasisi hiyo ikiwamo kutofanyia matengenezo miundombinu chakavu ya usafirishaji maji kutoka kwenye vyanzo hadi kwenye matangi ya kuhifadhia maji.

"Mtendaji Mkuu (Kiula) changamoto hii ya uzalishaji wa maji unaifahamu na nilishakupa maagizo ya kuchukua hatua tena nilikutajia majina, lakini hujachukua hatua, matokeo yake mnafanya kazi kirafiki 'kishikaji.'

"Nilikuagiza ukaonane na katibu mkuu kwa zaidi ya mara tatu hukuwahi kufanya hivyo na katibu mkuu alifanya ziara hapa viongozi hamkuonekana kirahisi tu," alisisitiza.

Aidha, alisema kushindwa kufanya matengenezo wakati kila mahitaji yapo, ni hujuma zinazolenga kuiharibia serikali kwa wananchi wake wanaolalamikia maji kila uchwao.

"Lazima nichukue hatua, bodi nawaomba msimamisheni Mhandisi Shaban (Mkurugenzi wa Uzalishaji na Usambazaji Maji wa DAWASA) na tutafuatilia kwanini uzalishaji anaosema hauakisi kwenye matangi ya kuhifadhia maji. Kama maji mtoni yapo na umeme upo kwanini maji kwenye matangi hakuna na watu hawapati maji," alihoji Aweso.

"Bodi naomba pia msimamisheni Mtendaji Mkuu kwa kushindwa kutekeleza wajibu wake, nilimwagiza lakini yupo kimya anafanya kazi kindugu wanashindwa kutambua tunawalipa mshahara kwa kodi za watanzania," alisema.

Aweso alimuhoji Mkurugenzi wa Uzalishaji na Usambazaji Maji wa DAWASA, Shaban Mkwanywe mbele ya waandishi wa habari na mahojiano hayo yalikuwa hivi:

**Aweso:** Waeleze wenzako, tumefika Chuo Kikuu Ardhi, tangi la lita milioni 40, maji yapo?

**Mkwanye:** Hayakuwapo

**Aweso:** Tumetoka pale, tumekwenda kwenye 'flow meter, flow inhalers' zinafanya kazi?

**Mkwanye:** Hazifanyi kazi Mheshimiwa.

**Aweso:** Lakini tumemkuta mtu anaandika kwenye kitabu juu ya uzalishaji maji, anaandika data kutoka wapi wakati 'flow meter' hazifanyi kazi?

**Mkwanye:** Sielewi Mheshimiwa.

**Aweso:** Tumeenda Kibamba, tangi lina lita ngapi?

**Mkwanye:** Milioni 10

**Aweso:** Haya embu tuambie ndani kuna lita ngapi pale?

**Mkwanye:** Kulikuwa hakuna maji.

**Aweso:** Kwa ukali; Lita ngapi sema!?

**Mkwanye:** Ziro.

**Aweso:** Sasa kama maji hakuna, malalamiko yatakuwepo, hayatakuwepo?

**Mkwanye:** Yatakuwapo.

**Aweso:** Nani anahusika na uzalishaji?

**Mkwanye:** Ni mimi Mheshimiwa.

**Aweso:** Ili tuwe na uzalishaji tunahitaji mambo mawili, la kwanza lazima tuwe na maji kwenye chanzo kwa maana ya mito, maji yapo, hayapo?

**Mkwanye:** Yapo Mheshimiwa.

Alisisitiza kuwa serikali imewekeza fedha kwenye utekelezaji wa miradi ya maji Dar es Salaam, Ruvu Juu na Chini ili watu wapate maji.

"Jukumu la DAWASA watu wapatiwe majisafi na salama, umeme upo, maji yapo, hatuna kisingizio, Kwanini maji kwenye matangi hayapo? Kwanini nisiwaombe polisi kukukamata kwa sababu umeme upo, maji yapo, kwanini wewe na timu yako nisiwaweke ndani?" Alihoji.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Jenerali mstaafu, Davis Mwamunyange, alisema katika ziara waliyofanya maeneo machache wamepata picha halisi.

"Hali ya utoaji huduma ya maji kwakweli ni mbaya na ziara ilikuwa ya kushtukiza na aliyofanya katibu mkuu ilikuwa ya kushtukiza zinafaa zaidi kuliko zile rasmi kwakuwa watendaji wanakuwa wamejiandaa," alisema Mwamunyange na kuongeza;

"Mimi sikutarajia na wajumbe wenzangu wa bodi tutakuta hali hiyo imetushtua. Ni jambo ambalo hatukulitarajia na hatua za haraka zinapaswa kuchukuliwa," alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mwajuma Waziri, alisema uwajibikaji wa watendaji wa DAWASA hauridhishi huku akieleza maji yanayopotea ni mengi.

Ziara ya Aweso imefanyika baada ya ziara ya Katibu Mkuu wa Maji aliyoifanya kwa siku mbili kujionea utendaji kazi wa DAWASA na hali ya upatikanaji wa maji.

Aidha, alibaini kuwapo uzembe aliouwasilisha kwa waziri ikiwamo miundombinu ya maji kuwa chakavu, maji kupotea bila usimamizi, watendaji wa DAWASA wa ngazi za chini kutopewa stahiki zao muhimu na kusababisha kufanya kazi bila hamasa nzuri na hata kuwajibu vibaya wateja.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe MWANGA WA JAMII The Guardian www.ippmedia.com

# WHO: Watanzania mil. 6/- hatarini kupofuka

**Na Faustine Feliciane**

ZAIDI ya watu milioni sita hatarini kuwa na upofu wa kudumu kutokana na kushindwa kupata huduma ya upasuaji wa mtoto wa jicho kwa wakati na kuamini wamelogwa.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, aliyasema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa Kituo cha Hisani cha Matibabu ya Macho cha KSI mkoani Dar es Salaam.

Alisema baadhi ya maeneo nchini kumekuwa na imani potofu kwa wananchi kwamba kufanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho watakuwa vipofu jambo linalo hatarisha afya zao.

"Napenda jamii ielewe kuwa hii si kweli na lazima elimu itolewe kwa watu kujua umuhimu wa kuwahi matibabu hasa ya mtoto wa jicho," alisema Ummy.

Aidha, alisema takwimu za Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa (WHO) zinaeleza kwa Tanzania watu milioni 12 hawana uhakika wa kupata huduma sahihi ya macho hususani maeneo ya vijijini.

"Hii inaonyesha bado hatuwajafikia watanzania wengi katika kuwapa huduma za macho, lakini pia takwimu hizo zinaeleza kati ya watu hao milioni 12, milioni sita wapo hatarini kupata upofu wa kudumu kwa kukosa matibabu ya haraka ya upasuaji wa mtoto wa jicho," alibainisha Waziri Ummy.

Alisema juhudi zaidi zinatakiwa kufikisha huduma hizo vijijini kwa kuhakikisha elimu inatolewa ili wawahi kupata huduma ya macho, ikiwa ni pamoja na upasuaji wa mtoto wa jicho.

Alisema serikali itaendelea kufanikisha upatikanaji wa huduma bora ya afya ikiwamo ya macho kwa wananchi kushirikiana na wadau wengine.

Alisema hadi sasa imeongeza wataalamu wabobezi wa magonjwa ya macho kutoka 55 mwaka 2016 na kufikia wataalamu 96.

"Serikali tunaishukuru sana taasisi hii ya KSI kwa kuona umuhimu wa kuwasaidia watanzania kupata huduma bora ya afya macho, tutaendelea kuunga mkono juhudi hizi zinazofanywa na taasisi binafsi," alisema.

Mwenyekiti wa KSI, Anverali Rajpar alisema kituo hicho kimejikita kutoa huduma na kuwasaidia watanzania wenye matatizo ya macho.

"Tunaishukuru Serikali ya Tanzania kwa kuweka mazingira mazuri ya utoaji huduma za afya, lakini pia tunashukuru wadau wengine kwa kuungana nasi kufanya kambi ya matibabu ya macho," alisema Rajpar.

# Manji azikwa Marekani, Yanga wamlilia

**Na Adam Fungamwango**

ALIYEKUWA mdhamini, mfadhili na Mwenyekiti wa Klabu ya Yanga, Yusuph Manji, aliyefariki Juni 29, mwaka huu jijini Florida, Marekani, amezikwa jana nchini humo.

Aidha, Klabu ya Yanga imesikitishwa na kifo hicho, ikisema alikuwa ni mwanamapinduzi wa soka nchini na shujaa aliyependa maendeleo ya sekta hiyo.

Taarifa iliyotolewa jana na mtoto wa marehemu, Mehbub Manji, ilieleza kuwa angezikwa jana saa tisa alasiri Orlando Florida karibu na sehemu aliyozikwa baba yake.

Wakati huo huo, Klabu ya Yanga imesema Manji alikuwa mmoja wa watu waliobadilisha Soka la Tanzania kutoka kuonekana kama la ridhaa zaidi na kuwa la kulipwa.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe alisema klabu ya Yanga imesikitishwa na kifo cha mfanyabiashara huyo maarufu ambaye alitumia nguvu, pesa na ushawishi wake kuboresha timu hiyo na kubadilisha mfumo wa uendeshwaji wa kuwa wa kisasa.

Alisema kwa wanachama wa klabu hiyo, Manji alikuwa ni mwanamapinduzi mkubwa katika mpira wa miguu ambaye alishiriki kwa hali ya mali kuhakikisha klabu inakuwa bora ndani na nje ya uwanja.

"Kwa niaba ya uongozi wa Yanga, Kamati ya Utendaji, tumepokea kwa masikitiko taarifa hii ya kifo cha Yusuph Manji ambaye alikuwa mdhamini, mfadhili na mwenyekiti wa klabu yetu.

"Hadi umauti unamkuta alikuwa mwanachama wa klabu yetu, hivyo tunatoa pole kwa ndugu, jamaa marafiki na wanamichezo wote kwa ujumla kwa sababu huu siyo msiba wetu tu, unaigusa sekta ya michezo," alisema Kamwe.

Akizungumza kutoka nchini Uholanzi, mmiliki wa klabu ya African Lyon, Rahim Zamunda, alisema Manji pamoja na kutoka Yanga, bado aliendelea kuwa na mapenzi na klabu hiyo na alisafiri kutoka nchini Marekani kwenda Afrika Kusini kuangalia mechi ya marudiano ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika katika ya timu yake dhidi ya Mamelodi Sundowns.

Taarifa za kifo hicho cha Mkurugenzi huyo wa Kampuni ya Quality Group Limited, na Diwani wa zamani wa Kata ya Mbagala Kuu kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), zilitolewa juzi usiku na mtoto wake.

Mfanyabiashara huyo atakumbukwa zaidi na wanachama na mashabiki wa timu hiyo kwa kumaliza mgogoro wa muda mrefu kati ya makundi mawili hasimu, Yanga Asili na Yanga Kampuni na kuirudisha kwenye hadhi yake.

Aliingia Yanga mwaka 2006 kama mdhamini kupitia kampuni yake moja ya bahati nasibu, baadaye mfadhili Mkuu wa klabu, kabla ya kuwa Mwenyekiti.

Moja ya wachezaji ambao timu hiyo iliwasajili kwa kishindo ni kutoka kwa mahasimu wao wa jadi Simba, Emmanuel Okwi, Kelvin Yondani, Juma Kaseja. Kisha ikawapora mchezaji, Mbuyu Twite ambaye alikuwa ameshatangazwa kuwachezea Wekundu wa Msimbazi hao kutokea, APR ya Rwanda









**HABARI KITAIFA**

# Wadau wa sukari wataja mkakati kuongeza uzalishaji

**Na Gwamaka Alipipi**

UMOJA wa Wazalishaji Sukari Tanzania (TSPA), umesema uzalishaji wa bidhaa hiyo unaoendelea sasa unatarajia kufikia tani 528,000 hadi 663,000 mwaka 2025/26, hali itakayoondoa nakisi ya bidhaa hiyo mwishoni mwa 2024/25.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kwa niaba ya wazalishaji wa sukari nchini, Balozi Ami Mpungwe, alisema baada ya kuwapo kwa vurugu kwa kipindi kirefu katika sekta ya sukari, kumekuwa na ongezeko kubwa la uzalishaji kutoka tani 293,146 mwaka 2015 hadi 460,200, mwaka jana.

Balozi Mpungwe alisema uzalishaji wa sukari umepunguza nakisi kutoka tani 144,000 mwaka 2017 hadi tani 30,000 mwaka 2023.

Alisema katika kuondoa nakisi ya sukari ifikapo mwishoni mwa mwaka 2024/25 na kwa uzalishaji unaoendelea hivi sasa, unatarajia kufikia tani 528,000 na tani 663,000 kwa mwaka 2025/26.

Balozi Mpungwe ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bodi wa Kiwanda cha Sukari Kilombero, alisema mojawapo ya jitihada walizozifanya za kupunguza uhaba wa sukari nchini ni kuagiza tani 4,500 kutoka nje wakati wa uhaba.

"Kilombero tulileta kiasi hicho cha sukari kabla ya kupewa kibali, tulipopewa kibali tukaagiza tani 5,000 kutoka Brazil. Hivyo sio kweli kwamba tulikataa kupokea vibali au tuliviuza kwa wengine," alisema balozi Mpungwe.

Aidha, wazalishaji hao wamelalamikia hatua ya serikali kutowashirikisha katika mjadala, hatua na maamuzi yanayochukuliwa katika sekta ya sukari, ikiwamo utoaji wa vibali vya kufidia nakisi.

Pia, wamelalamika kutupiwa lawama za kusababisha kukwamisha uzalishaji na usambazaji wa sukari nchini, hata kupewa majina mabaya, wakisema hatua hiyo inalenga kuichafua na kudhoofisha sekta na kampuni za kuzalisha sukari.

Kwa mujibu wa Balozi Ami Mpungwe, wanapewa lawama zisizo na ukweli, lakini hawajapewa nafasi ya kusikilizwa.

"Tulitegemea tungeitwa tusikilizwe, lakini kimya. Tulifanya jitihada za kuandika barua kwa Spika wa Bunge hususani wakati mjadala ulipopamba moto bungeni, lakini hatukuitwa ila tumeambiwa twende Bunge la Agosti," alisema na kuongeza:

"Tulitaka kuwaeleza namna hali ilivyo. Hata bei ya sukari ilipopanda hatukusababisha sisi bali ni sokoni. Lakini vidole tulinyooshewa sisi," alisema Balozi Mpungwe.

Kadhalika, sekta ya sukari imeyumba kwa miaka mingi, na kumekuwa na vurugu, akitoa mfano utawala wa Hayati Rais John Magufuli, serikali ilisimamia kidete sekta ya sukari na ilipiga marufuku uagizaji holela akisema lengo lilikuwa ni kulinda afya za Watanzania.

Kutokana na hatua madhubuti zilizochukuliwa na serikali za kuvilinda viwanda na wakulima wa miwa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, hivi sasa viwanda vyote vinafanya upanuzi wa kilimo cha miwa na uchakataji wa sukari.

Alisema viwanda vya sukari nchini, kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita vimewekeza Sh. trilioni 3.5, uwekezaji mkubwa unaoongoza katika sekta ya kilimo nchini, ambao pia umekuwa chachu ya uhamasishaji na kuvutia wawekezaji wengi.

Kuhusu Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) kupewa mamlaka ya kuhifadhi, kuagiza sukari kutoka nje, Balozi Mpungwe alisema ni uamuzi mzuri na wanaunga mkono, lakini alitoa angalizo kusitokee wajanja wakatumia fursa hiyo kujinufaisha

Naye Mkurugenzi wa Kiwanda cha Sukari Bagamoyo, Hussein Sufian, alisema awali serikali iliwapatia vibali vya kuagiza sukari tani 50,000 jambo ambalo walilitekeleza.

Alisema TSPA hawazitambui wala kuzifahamu kampuni zingine zilizopewa vibali vya kuagiza sukari, kwamba sukari inayoagizwa na kampuni hizo inauzwa bei ndogo kuliko ile inayozalishwa nchini kwa sababu hawalipi ushuru wala Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Nipashe lilimtafuta Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe ili kupata ufafanuzi wa malalamiko hayo, hata hivyo simu yake iliita pasipo kupokelewa na hata alipotumiwa ujumbe mfupi wa maneno hakujibu.

## Mbowe awajibu wanaokihama chama

**Na Godfrey Mushi,** HANDENI

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amewajibu wanasiasa wanaokihama chama hicho na kumshambulia, huku akiwataka Watanzania kutokiangalia chama hicho kwa sura ya Mbowe.

Bila kumtaja mtu, alirusha dongo kwa wanaokitazama kwa sura hiyo, akiwataka wanaomshambulia pamoja na Watanzania wengine kuiangalia CHADEMA kwa mambo inayoyasimamia.

Akizungumza jana na wananchi wa Kabuku, Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga, anakoendelea na operesheni iliyobatizwa jina la Operesheni GF alisema:

"Chama hiki sio cha Mbowe. Mmejenga chama chenu na chama hiki leo kimekuwa nchi nzima. Samia anajua (Rais Samia Suluhu Hassan), Majaliwa anajua (Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa). Nyie wananchi wa Tanga msikiangalie CHADEMA kwa sura ya Mbowe.

"Kiangalieni CHADEMA kwa mambo ambayo inayokisimamia. Chama hiki kina misingi minne. Msingi wa kwanza, ni haki kwa watu wote, haki kwa watoto, haki kwa wamama, haki kwa wababa, haki ya kuabudu, haki ya kila mmoja aheshimiwe kwa nafasi yake.

...Ndani ya serikali ya CCM, watu wamebanwa kila mahali michango, kila mahali manung'uniko, kila mahali uonevu,kila mahali viposhopo-sho sijui vimichango michango. Mtendaji wa Kata anakuzonga, Mwenyekiti wa Kijiji anakuzonga, uongo kweli? Tunataka tujenge taifa la watu huru, furaha."

Akionyesha kuchukizwa na wanaokikosoa kwa kukitazama CHADEMA kwa sura yake, Mbowe, alisema wanapaswa kutazama msingi wa tatu, ambao ni chama ambacho kina msingi wa kuamini viongozi wa watu wapatikane kwa kura za wengi.


NMB
Close to you

**REQUEST FOR INFORMATION (RFI)
SUPPLY AND INSTALLATION OF INTEGRATED BUSINESS MANAGEMENT SYSTEM.**

1. NMB Bank Plc is the largest commercial bank in Tanzania with vast branch network in all parts of the country, providing banking services to individuals, small and medium size corporate clients, as well as large businesses.
2. NMB Bank Plc now invites applications for submission of information from all eligible vendors for the Supply and Installation of ***Integrated Business Management System.***
3. This RFI is issued for the purpose of obtaining information concerning market conditions and vendor's capability. The Bank does not intend to award a contract on the basis of this solicitation or to otherwise pay for the information solicited. The Bank reserves the right to defer or cancel the RFI without penalty.
4. NMB Bank Plc is expecting to receive technical information, which showcase both high level functional and non-functional system capabilities.
5. The Selection and shortlisting of vendors for future RFP process will be conducted through the Open Competitive Tendering as specified in the NMB Bank Plc Procurement Policy and Procedures. After receiving the information through proposals from interested vendors, the Bank will review and invite the selected vendors to showcase/present what their system has to offer.
6. RFI document shall be obtained from our website **www.nmbbank.co.tz/tenders** and request for clarifications sent to the office of Secretary, Management Tender Committee at **procurement@nmbbank.co.tz** not later than Wednesday 03rd July 2024.
7. The deadline for submission of the applications will be on **Monday 08th July 2024 at 15H00 EA Time.** Applications received will be opened promptly thereafter and in the presence of vendor's representatives who will choose to attend in the opening ceremony at NMB Bank Plc Head Office on the first floor at 15H00 EA Time on Monday 08th July 2024.

The application shall be addressed to Secretary NMB Bank Plc. Management Tender Committee and clearly marked on the envelope/email: **RFI for Integrated Business Management System Not to be opened before 15H00 on Monday 08th July 2024** and delivered in the following ways: -

- In a sealed envelope hand delivered or couriered to **NMB Bank Plc Head Office Ohio Street/Ali Hassan Mwinyi Road, P O Box 9213, Dar es Salaam, Tanzania** at the ground floor,
- Via email to **tendersubmission@nmbbank.co.tz** (maximum 25MB).

**The Chief Executive Officer, NMB Bank Plc
P.O. Box 9213, Dar Es Salaam, Tanzania, East Africa
NMB Head Office Ohio/Ali Hassan Mwinyi Street**

***www.nmbbank.co.tz***

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Funguo, msako madalali ufanikishe NHC mpya

**MADALALI** wa nyumba za Shirika la Nyumba Tanzania (NHC), waliokuwa wakitamba mjini kwa kuwapangisha wengine kwa gharama kubwa na kujinufaisha, arobaini zao zimetimia.

Ni baada ya serikali kuliagiza shirika hilo kufanya operesheni ya kuwaondoa watu wanaofanya udalali na kwa na sasa NHC inaandaa mikakati ya msako huo nchi nzima.

Ni hatua mahususi ya kuwezesha nyumba hizo kubakia kuwa mali ya umma na zisiendelee kugeuzwa kuwa vitega uchumi na miradi ya watu wachache wanaojinufaisha tena kwa fedha nyingi.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geoffrey Pinda, ndiye anayetoa maelekezo na kuagiza hatua hiyo ichukuliwe baada ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kutembelea miradi ya shirika hilo jijini Dar es Salaam.

NHC imekuwa moja ya eneo ambalo watu wanajinufaisha hasa kutokana na uhitaji wa makazi bora na kwa gharama nafuu.

Ni wazi kuwa kuna wakati shirika hilo lilitangaza kuwa lingetoa ufunguo wa kielektroniki kama 'LUKU' ambao kama mteja hajalipa kodi mlango ungejifunga, yote hayo yakilenga kuzuia kuchelwesha malipo.

Hatua ya kutoa ufunguo ingeendana na kuwatambua wapangaji halali na kuwatambua kwa vitambulisho halali kama vya taifa, pasi za kusafiria na alama za vidole hata hivyo bado hakuna kilichosikika kuhusu mkakati huo, ambao NHC wanafahamu kinachoendelea.

Kuna haja ya kuliendesha shirika hilo kwa ubunifu na hata kielektroniki lakini si nyumba za NHC tu pengine hata za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) , ambazo nazo kuna madai kuwa kuna wajanja wanazifaidi.

Kama anavyowakumbusha Naibu Waziri, serikali inataka wapangaji wa nyumba hizo wajulikane ili waweze kupewa upangaji rasmi badala ya kuwa wanalipa fedha nyingi kwa watu ambao hawahusiki na nyumba hizo.

Tunaona hatua hiyo ni muhimu na itasaidia kuwapunguzia gharama kubwa ambazo baadhi ya wapangaji wa nyumba hizo walikuwa wanakumbana nazo kutokana na ujanja unaofanywa na watu wachache.

Kwani kwa mujibu wa Naibu Waziri, serikali inafahamu kuwa watu wanachukua fedha nyingi kwa kupangisha wengine, jambo ambalo ni wazi wapangaji wanaumia lakini wajanja wakinufaika.

Kitendo cha baadhi ya watu kuchukua nyumba zaidi ya 10 na kupangisha wananchi kwa gharama kubwa ni sawa na kuwaumiza na kufanya wengine kuziona nyumba hizo kama ni mali binafsi au zinazoendeshwa kijanja licha ya kuwa ni mali ya umma.

Lakini pia tunadhani kitendo hicho kinaweza kusababisha wapangaji kushindwa kulipa pango kwa wakati kwa NHC lakini wakiwanufaisha matapeli kutokana na ukweli kwamba wanawahofia madalali kuliko mmiliki halali.

Ni miongoni mwa mambo yanayolisababishia shirika hasara au hata kushindwa kukamilisha miradi yake kwa wakati kutokana na ukosefu wa fedha zinazotoka kwa wapangaji wake.

Hivyo, uamuzi wa kuwaondoa wanaofanya udalali wa nyumba za NHC ni hatua bora ambayo pengine ilichelewa .

Ni vyema pia NSSF ikaliangalia hilo na kuchukua hatua kama ambavyo shirika la nyumba limefanya ili kujihakikishia mapato yanayovuja kwa njia kama hizo za madalali.


Tunaamini kwamba msako huo ukifanyika kikamilifu, utakuja na matokeo chanya ambayo yatasaidia shirika kuwa na wapangaji sahihi watakaolipa kodi na kuchangia kuendeleza na kuimarisha NHC kimapato.

Hatuna maana kwamba waliomo sio sahihi, bali inawezekana walipatikana katika mazingira hayo ya udalali na kufanya fedha nyingi kuishia kwa madalali, huku shirika likipata kidogo.

Kwa maelekezo hayo ya serikali kutaka shirika lianzishe msako, tunaona kuwa inawezekana ikawa suluhisho la kudumu ili NHC ipate wapangaji halali watakaolipa kodi kwa wakati.

Lakini pia, iwe ni fursa kwa watu wenye kipato cha kawaida kutumia nyumba hizo badala ya kuziona kuwa ni za watu wa tabaka la juu kwa maana ya wenye kipato kikubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Sabato Kasika

# Muungwana Lazima Nilonge

## Simu ni muhimu shuleni ikitumika vizuri

**MOJA** ya masharti katika fomu za wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza kwenye baadhi ya sekondari, ni kuonywa kuwa hawaruhusiwi kuwa na simu shuleni na pia mtumishi au mwalimu ni marufuku kutunza simu za wanafunzi.

Suala hilo la baadhi ya shule kukataza simu shuleni, limeibua mjadala katika jamii, wakiwamo watu wanaoona si vibaya kuwa na simu na wengine wakiunga mkono katazo hilo.

Watu wasiishi kwa mazoea nadhani ipo haja ya kulegeza masharti ambayo yanawabana wanafunzi kuhusu matumizi ya simu wawapo shuleni, hasa kutokana na kwamba katika karne ya sayansi na teknolojia, matumizi ya simu yamekuwa ni muhimu hata kwa wanafunzi.

Kwa kutumia mfumo wa Teknolojia , Habari na Mawasiliano (TEHAMA), unaweza kuwasaidia wanafunzi kupata vitabu vya kujifunzia unaofahamika kama Maktaba Mtandao kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

Ili mwanafunzi aweze kuupata na kuutumia, ni lazima atumie kifaa kama simu , kompyuta au kishikwambi, hivyo ni wazi kwamba kuna umuhimu wa kulegeza masharti ili wanafunzi watumie simu shuleni.

Jambo la msingi ni kuweka utaratibu wa kuhakikisha hawavitumii kwa mambo mengine yasiyoendana na elimu. Simu zitunzwe sehemu moja ili mwanafunzi anapohitaji kuitumia kupakua vitabu, apewe kisha arudishe.

Hapa maana yake ni kwamba mwanafunzi asiende na simu shuleni kwa kificho, bali kila mwanafunzi ajulikane na kuelekezwa jinsi ya kuzitumia, ili waweze kufaidika na TEHAMA.

Ninaamini kwamba kwa kuzingatia matumizi ya sahihi ya simu janja, kuna faida nyingi kuliko madhara hasa kipindi hiki ya sayansi na teknolojia ambacho kila kitu kiko mtandaoni.

Kimsingi, shuleni ni mahali ambako kuna sheria, kanuni na taratibu wake, hivyo kila jambo likisimamiwa ipasavyo kwenye matumizi sahihi ya simu janja wanafunzi wanaweza kufanya vizuri katika masomo.

**Hapa maana yake ni kwamba mwanafunzi asiende na simu shuleni kwa kificho, bali kila mwanafunzi ajulikane na kuelekezwa jinsi ya kuzitumia, ili waweze kufaidika na TEHAMA.**

Ninadhani si vibaya kama simu zikiwa maslumu kwa ajili ya0 wanafunzi kwa kuwekwa program zinazohusiana na masomo yao tu badala ya kuangalia programu nyingine zinazoweza kuwaweka katika matatizo.

Ninatambua kuna sababu mbalimbali zinazochangia kuzuia shuleni, ikiwamo kuhofia wanafunzi kufeli kutokana na kuendekeza simu zaidi kuliko masomo. Hilo ni kweli hasa simu zikitumiwa vibaya.

Lakini ikumbukwe kuwa kwa sasa simu sio chombo tu cha kuzungumza bali pia ni chenye zana mbalimbali muhimu katika maisha ye kila siku, hivyo ni vyema tuakaendana kulingana na taknolojia ilivyo.

Kama yapo ambayo tumerithi kutoka kwa wakoloni na tunaamini yamepitwa na wakati, basi hatuna budi kuyaacha, ili wanafunzi waweze kuonyesha ujuzi wao kupitia TEHAMA, lakini kwa kuwasimamia.

Suala la matumizi mazuri au mabaya ya simu, yako pande zote kwa watoto (wanafunzi) na hata watu wazima, hivyo jambo la msingi kwa wanafunzi na kuwafundisha matumizi sahihi na kuwasimamia.

Ninaamini kuna haja ya kuruhusu matumizi ya TEHAMA kwa faida ya wanafunzi, walimu, shule na jamii husika kwa ujumla. Jambo la kuzingagtia ni usimamizi. Kila mwanafunzi mwenye simu ajulikane na aitumie kwa wakati maalum awapo shuleni.

Ukiwapo usimamizi, ni wazi mwanafunzi hatatumia simu kwa mambo binafsi, badala yake ataitumia kwa ajili ya mambo ya shule tu.

Wale watakaoshindwa kufuata utaratibu, basi wasiruhusiwe kuwa nazo.

Kwa sasa somo la TEHAMA yanafundishwa shuleni, hivyo wanafunzi wataendelea kuzuiwa kuwa na simu shuleni, wataendeleo kubaki nyuma, hasa kutokana na ukweli kwamba sio kila shule ina komyuta za kutosha kufundishia somo hilo.

# DC asitisha mkataba wa shirika/kijiji madai ukiukwaji

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Mvomero, mkoani Morogoro, Judith Nguli amesitisha mkataba wa uboreshaji wa maeneo ya msitu uliosainiwa kati ya Kijiji cha Gonja na Shirika linalojihusisha na Uendelezaji wa Maeneo ya Misitu kwa ajili ya kurudisha uoto wa asili la PAMS Foundation, kwa madai mkataba huo ulikiuka taratibu muhimu.

Aidha, mkataba huo ulilenga kuendeleza eneo lenye ukubwa wa ekari zaidi ya 1,900 na ulisha sainiwa baina ya pande zote mbili.

Akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Gonja, Nguli alisema serikali imesikia malalamiko yao wakidai kugomea mkataba huo kwa sababu makubaliano waliyoafikiana awali yamekiukwa na hivyo kusitisha mkataba huo na kuagiza kusainiwa upya ndani ya wiki mbili kati ya pande hizo mbili.

Alisema upungufu uliopo kwenye mkataba huo ukiwamo wa kutokuwapo kwa ushirikishwaji wa wananchi wakati wa mabadiliko ya fedha kutoka Sh. milioni 180 waliyoahidiwa awali na kupewa Sh. milioni 34, Shirika la PAMS halikufanya tathmini ya kina kujua ukubwa wa eneo linalotakiwa kufanyiwa maboresho.

Kutokana na upungufu huo, Mkuu huyo wa wilaya amelazimika kusitisha mkataba huo pamoja na shuguli zote kwenye eneo la msitu.

"Nasitisha shughuli zote kuanzia sasa zisimame zisiendelee kwanza mpaka mwafaka wa makubaliano ya pande zote mbili yatakapofikiwa ikiwa ni pamoja na kusainiwa upya mkataba," alisema.

Aliagiza Sh. milioni 34 zilizolipwa na shirika hilo zisitumike hadi mwafaka utakapofikiwa baada ya wiki mbili, huku akitaka wananchi washirikishwe tathmini itakapofanyika.

Pia, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, ameagizwa kuwachukulia hatua za kinidhamu waliohusika na usumbufu huo ili liwe fundisho kwa watumishi wengine.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Shirika la PAMS Foundation, Elisifa Ngowi, alithibitisha kuwapo kwa kasoro katika tathmini ya eneo pamoja na ushirikishwaji wa wananchi kwenye mabadiliko ya fedha.

Alisema shirika hilo linajihusisha na uendelezaji wa maeneo ya misitu iliyoharibiwa kwa kupanda miti ili kurudisha uoto wa asili kama ilivyokuwa awali na katika msitu wa Kijiji cha Gonja zaidi ya ekari 300 kati ya 1,900 ndizo waliingia mkataba wa kuziendeleza.

Ofisa Maliasili Mkoa wa Morogoro, Joseph Chuwa, alisema mkoa huo una misitu ya vijiji 109 ambayo ina sifa ya kupata miradi ya uwekezaji wa hewa ya ukaa, lengo la uwekezaji huo ni kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo kwa hivi karibuni dunia imeshuhudia athari zake ikiwamo mafuriko, vimbunga na ongezeko la joto.

Chuwa alisema kutokana na umuhimu wa misitu hiyo kwa sasa elimu inatakiwa kutolewa kwa wananchi waelewe uwekezaji huo.

Kwa mujibu wa mkataba huo Kijiji cha Gonja kitapata Sh. milioni 34 kila mwaka kutoka kwa PAMS Foundation kwa kipindi cha miaka 30, ikiwa ni mapato yatokanayo na kukodisha msitu huo.




Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Riziki Shemdoe (kushoto), akikabidhi cheti kwa mmoja wa wahitimu 30 wa mafunzo ya masuala ya mifugo na utafiti wa magonjwa ya wanyama kwenda kwa binadamu, yaliyoandaliwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na kufadhiliwa na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), mjini Morogoro, mwishoni mwa wiki. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

# Othman Masoud aasa waislam kujenga mwenendo mwema

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema wajibu wa kuendeleza elimu ya dini ya Kiislamu nchini wanaopaswa kuwa mstari wa mbele ni waislamu wenyewe.

Aliyasema hayo mkoani hapa alipomwakilisha Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, katika mahafali ya 67 ya Jumuiya ya Chuo cha Ualimu wa Kiislamu Tanzania (TAMTA), iliyofanyika katika viwanja vya Madrasat Shamsiyya, Msambweni.

Masoud alisema kufanya hivyo ni muhimu kwa kuwa elimu ya dini ya usilamu kupitia mafunzo ya kitabu kitakatifu cha Qur'aan ndio iliyobeba taaluma zote zinazofundishwa ulimwenguni zikiwamo za sayansi, ufundi na tiba mbali mbali kwa binaadamu.

Aidha, alisema suala hilo ni muhimu kutokana na elimu ya uislam inaendelea kutoa mafunzo makubwa katika kujenga mwenendo mwema wa maisha ya mwanadamu ili aishi kwa imani na nchi kuwa na amani na maendeleo.

Aliwataka waislamu nchini kuwa na mifumo pia na hombo sahihi na madhubuti cha kusimamia haki za waislamu na uislamu wa Tanzania ikiwamo zaka ili kujenga nafsi za wauumini nchini ziweze kunyooka.

Aliukumbusha uongozi wa Jumuihiyo pamoja na waislamu nchini haja ya kuungana ili kukikuza chuo hicho kukifanya kuwa ni taasisi imara na bora zaidi yenye mifumo na taratibu sahihi za kuakisi mahitaji ya kuendeleza dini ya kiislamu nchini na kufika mbali zaidi kiuwezo na taaluma kuliko ilivyo sasa.



Alimpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake na uongozi mwema na mahiri wa kuisaidia nchi kuwa na amani na utulivu na wananchi kuendelea kuitamani kesho ifike ili waendeleze kufanya shughuli zao za maendeleo.


Mufti Mkuu wa Tanzania, Shekhe Abubakar Zubeir, alisema kwamba juhudi za waanzilishi wa Jumuiya hiyo zimesaidia kupatikana kwa mashekhe, wanazuoni na walimu bora ambao hivi sasa wamesambaa duniani wakiendeleza juhudi za kufundisha dini ya kiislamu.

Aidha, alisema hali hiyo imeifanya nchi kuwa mashuhuri katika masuala ya dini na kuwataka waislamu nchini kuendelea kuungana na kushirikiana vyema kukiendeleza chuo na madrasa za aina hiyo ikiwa ni pamoja na kuchangia kuimarisha mazingira ya chuo hicho katika kufundisha kwa mujibu wa hali ya sasa.

Awali, Othman alipokea maandamano ya vikundi mbali mbali vya kiislamu ambao ni mazao ya taasisi hiyo kutoka sehemu za Mkoa wa Tanga na mikoa mingine na kushuhudia maonesho ya umahiri na weledi wa ufahamu wa ya kiislamu kwenye fani tofauti.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Maonesho DITF kujikita teknolojia akili mnemba

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imesema Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ambayo yatakuwa na washiriki 3,846 yamejikita zaidi katika teknolojia ya hali ya juu, ubunifu na matumizi makubwa ya akili mnemba.

Maonesho hayo yaliyoanza Juni 28 yanatarajiwa kumalizika Julai 28 yanafanyika katika Uwanja wa Maonesho wa Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam.

Naibu Waziri wa Viwanda, Exaud Kigahe, aliwaambia waandishi wa habari kuwa mwaka huu wanatarajia kuwa na jumla ya washiriki 3,846, wa ndani ni 3,433, kampuni za ndani sekta binafsi 3,286, wizara nane, mikoa minne, halmashauri 30, taasisi za umma 105, nchi za nje 26, kampuni za nje 413 na watembeleaji 353,201.

Alisema maonesho hayo yanatarajiwa kutengeneza ajira za muda 11,712 na kwamba kwa mwaka jana kulikuwa na washiriki 3,500, wa ndani ni 3,233, washiriki wa nje 267, nchi za nje 19, watembeleaji 300,701 na ajira za muda 11,687.

"Hadi sasa tuna nchi 26 zilizothibitisha kushiriki katika maonesho haya, nchi hizo ni pamoja na Korea, Uturuki, India, Japani, Singapore, Syria, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Msumbiji, Indonesia, Mauritius, Oman, Misri, Iran, Pakistan, Rwanda na Comoro.

Alitaja nchi zingine kuwa ni Zambia, Ethiopia, Kongo DRC, Ghana, China, Urusi, Italia, Uganda, Kenya na Zimbabwe na nchi nyingi kati ya hizo zinakuja kuonesha teknolojia mpya za mashine mbalimbali.

"Teknolojia hizo ni zile zinazohitajika na Watanzania katika kuanzisha viwanda vikubwa, vya kati na vidogo, hivyo niwaombe wafanyabiashara wetu wa ndani watumie fursa hizi kujifunza kwa ajili ya kuongeza uzalishaji, ubora wa bidhaa pamoja na kupanua wigo wa masoko ya bidhaa zao," alisema Naibu Waziri.

Alisema kutakuwa na matukio maalum mbalimbali kama vile siku maalum za nchi saba zinazoshiriki kwenye maonesho hayo, ambazo ni China, Japan, Korea, Iran, Misri, Urusi na India na kutakuwa na programu ya Sabasaba urithi wetu.

Alisema kutakuwa na programu za mikutano ya ana kwa ana, siku za kampuni zinazojumuisha sekta mbalimbali ambazo zimeandaliwa kwa kushirikiana baina ya sekta binafsi na sekta ya umma zikiwamo TIC, ZIPA, TPSF, CTI, TCCIA na ZNCC.

Alisema lengo la siku hizi za kampuni ni kuwawezesha wafanyabiashara wa kitanzania kupata fursa ya masoko ya nje.

"Napenda kutumia nafasi hii kuwakaribisha Watanzania wote wenye vikundi vya ujasiriamali, kampuni, taasisi za umma na binafsi kushiriki kwenye maonesho haya kwa kuwa ni jukwaa muhimu sana la kukutana na wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kujifunza teknolojia mbalimbali," alisema.

Aidha, alisema washiriki watapata maarifa ya kisasa ya uzalishaji, ufungashaji na usambazaji wa bidhaa, kupata masoko ya ndani na nje pamoja na ajira.

Naibu Waziri alisema maonesho ya mwaka huu yamebeba kaulimbiu "Tanzania: Mahali Sahihi pa Biashara na Uwekezaji'.

Alisema kaulimbiu hiyo inalenga kuonesha dunia kuwa serikali iko tayari na inaendelea kuweka mazingira rafiki kwa wafanyabiashara na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kufanyabiashara na kuwekeza katika sekta mbalimbali za uzalishaji ikiwamo sekta ya viwanda, kilimo, teknolojia, uwekezaji na utalii.

Alisema mgeni rasmi katika maonesho hayo siku ya ufunguzi ni Rais wa Msumbiji, Filipe Jacinto Nyusi na kwamba Rais Samia ambaye ni mlezi mkuu wa maonesho ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam atashiriki pia katika ufunguzi wa maonesho hayo.




## Wasioona walalamika kuongezeka unyanyapaa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

CHAMA cha Watu Wasioona (TLB), kimelalamikia unyanyapaa unaoendelea dhidi yao, huku wakiiomba serikali kuingilia kati kwa kutoa elimu jamii ithamini kundi hilo ambalo linajishughulisha katika shughuli mbalimbali ikiwamo za biashara.

Kaimu Mwenyekiti wa chama hicho ngazi ya taifa, Habiba Ngulangwa, alisema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na Nipashe mjini hapa baada ya mafunzo ya ujasiriamali kwa baadhi ya wanachama wa chama hicho.

Alisema baadhi ya kundi hilo ni wajasiriamali wanaokumbana na unyanyapaa kwenye shughuli zao wakionekana hawafai kufanya kazi hizo na hawana uwezo nazo huku wakitamkiwa maneno ya kuwakatisha tamaa.

"Serikali izidi kutoa elimu kwa jamii kuhusu watu wenye ulemavu ili waelewe nasisi tuna uwezo kama wao na wapo wengine hawana ulemavu tumewazidi kwa akili na uendeshaji wa miradi," alisema.

Akizungumzia mafunzo hayo, Habiba alisema lengo ni kuwainua wasioona na yametolewa kwa kundi la vijana na wanawake waweze kujikwamua kiuchumi kupitia mikopo ya asilimia mbili inayotolewa kwenye halmashauri.

Kadhalika, aliiomba serikali kuzingatia haki wanazostahili kuzipata ili waweze kutekeleza malengo yao kama ilivyo kwa wengine ikiwa ni pamoja na kushiriki kikamilifu kwenye chaguzi zijazo.

Awali, Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Pwani, Lidya Mafole, aliwapongeza kwa kuandaa mafunzo hayo ambayo yatawawezesha kuwa na utaratibu mzuri wa kufanya shughuli zao za ujasiriamali.

Aliwasisitiza kuyatumia vizuri kuboresha shughuli zao huku akiwahakikishia ofisi yake kuendelea kushirikiana na ofisi za maendeleo ya jamii kwenye halmashauri kuhusu mwenendo wa mikopo itakapoanza kutolewa.

Kwa mujibu wa Mafole, wanaendelea kushirikiana na vyama vya watu wenye ulemavu kufanya utambuzi na mahitaji na shughuli zao kuingizwa kwenye mipango ya bajeti za halmashauri.

**TANGAZO**

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

# TAARIFA KWA UMMA

## MAKUSANYO YA KODI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Dares Salaam, 01 Julai, 2024:**
Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuufahamisha umma kuwa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/24, imefanikiwa kukusanya kiasi cha Shilingi Trilioni 27.64, ambayo ni sawa na ufanisi wa asilimia 97.67 ya lengo la kukusanya Shilingi Trilioni 28.30. Makusanyo haya ni ongezeko la asilimia 14.50 ikilinganishwa na makusanyo ya Shilingi Trilioni 24.14 katika Mwaka wa Fedha uliopita, 2022/23.

Katika kipindi cha robo mwaka ya nne yaani Aprili - Juni, 2024, TRA imefanikiwa kukusanya kiasi cha Shilingi Trilioni 7.09, sawa na ufanisi wa asilimia 99.46 ya lengo la kukusanya kiasi cha Shilingi Trilioni 7.13. Makusanyo haya ni ongezeko la asilimia 24 ukilinganisha na kiasi cha Shilingi Trilioni 5.72 kilichokusanywa katika kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha uliopita 2022/23. Jedwali Na. 1 linaonesha mlinganisho wa mwenendo wa makusanyo kwa kila robo ya Mwaka wa Fedha 2022/23 na 2023/24.

**Jedwali Na.1: Makusanyo ya Kodi Mwaka wa Fedha 2023/24.**

| Mwezi | 2022/23 | 2023/24 | | | Ukuaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | Makusanyo Halisi *(Milioni Shilingi)* | Lengo (Milioni Shilingi) | Makusanyo Halisi *(Milioni Shilingi)* | Ufanisi | |
| Robo ya Kwanza (Jul – Sep 2023) | 5,924,493.01 | 6,745,293.35 | 6,574,845.86 | 97.47% | 10.98% |
| Robo ya Pili (Okt – Des 2023) | 6,561,658.01 | 7,460,410.20 | 7,341,719.12 | 98.41% | 11.89% |
| Robo ya Tatu (Jan – Mac 2024) | 5,936,715.24 | 6,966,477.44 | 6,634,890.46 | 95.24% | 11.76% |
| Robo ya Nne (Apr – Jun 2024) | 5,715,589.31 | 7,125,289.72 | 7,087,140.82 | 99.46% | 24.00% |
| **Jumla (Ghafi)** | **24,138,455.57** | **28,297,470.72** | **27,638,596.26** | **97.67%** | **14.50%** |

**Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania**

**Ongezeko hilo la makusanyo katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/24 limechagizwa na:**

i. Ukuaji wa shughuli za kiuchumi nchini hususani uzalishaji viwandani na kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaotembelea nchini kujionea vivutio mbalimbali vilivyopo;
ii. Mwitikio mzuri wa walipakodi wengi katika kuwasilisha ritani na kulipa kodi kwa wakati;
iii. Kuongezeka kwa uhiari wa ulipaji kodi kufuatia maboresho yanayoendelea kufanywa na TRA ikiwemo uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA, kusogeza huduma jirani na walipakodi kwa kuanzisha Divisheni za Walipakodi Wadogo na Walipakodi wa Kati, pamoja na kuendelea kusuluhisha pingamizi za kodi nje ya mahakama; na,
iv. Kuongezeka kwa uingizwaji wa mizigo toka nje ya nchi kutokana na uboreshwaji wa mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini.

Pamoja na mafanikio haya, vitendo vya ukwepaji kodi na kutozingatia sheria vimeendelea kushamiri miongoni mwa makundi mbalimbali ya walipakodi ikiwemo watu binafsi, makampuni ya ndani na yale ya kimataifa. TRA itaendelea kuhimiza ulipaji kodi kwa kufuata sheria zilizopo na utekelezaji wake kuzingatia misingi ya utawala bora. TRA inaendelea kuhimiza matumizi ya njia ya majadiliano na maridhiano katika kuzuia na kutatua migogoro mbalimbali ya kikodi kwani mara nyingi njia hii imekuwa ikileta matokeo chanya yenye manufaa kwa pande zote. Hata hivyo, inapojitokeza migogoro isiyoweza kumalizwa kwa njia ya majadiliano, TRA inawahimiza walipakodi kutumia haki yao ya kisheria kwa kufuata utaratibu wa kushughulikia mapingamizi na rufaa za kodi uliopo kwa mujibu wa sheria hususani kupitia Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438 na Sheria ya Rufani za Kodi, Sura ya 408. Utaratibu huu utahakikisha migogoro ya kodi inatatuliwa kwa kufuata misingi ya sheria na haki kupatikana bila kuleta taharuki kwa jamii.

TRA inapenda kuwashukuru walipakodi na watanzania wote kwa ujumla kwa kuendelea kulipa kodi ikiwa ni njia muhimu ya kuunga mkono juhudi za kuleta maendeleo nchini zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kuendeleza hilo kwa vitendo, TRA inaendelea kutoa wito kwa walipakodi na wananchi wote kuendelea kutoa na kudai risiti za Kielektroniki (EFD) kwa kila manunuzi ya bidhaa au huduma, kuhakiki uhalali wa stempu za kielektroniki za kodi (ETS) katika bidhaa, kuwasilisha ritani na kulipa kodi stahiki kwa wakati, kutoa taarifa za vitendo vya ukwepaji kodi pamoja na kuzingatia matakwa mengine ya sheria za kodi. Hii itaongeza uwezo wa Serikali kuendesha shughuli mbalimbali za kuleta maendeleo nchini ikiwemo utekelezaji wa miradi kama vile ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, maji na uboreshaji wa huduma za jamii kwa ustawi wa maisha ya Watanzania.

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Kidatah

**A.J.Kidata**
**Kamishna Mkuu**





# RC Macha aanika uozo wa madiwani mikopo 10%

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha ameanika vitendo vya uvunjifu wa sheria za mikopo ya asilimia 10 ya halmashauri vinavyofanywa na baadhi ya madiwani mkoani humo, ikiwa ni pamoja na kuunda vikundi binafsi ambavyo havirejeshi fedha hizo.

Macha alibainisha hayo juzi katika kikao maalumu cha baraza la madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Kahama cha kupitia na kujadili hoja mbalimbali za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2022/2023, na kupata hati safi baada ya kujibu kikamilifu hoja 25 za mwaka huo.

Alitaja moja ya kesi aliyokutana nayo kuhusu diwani (jina limehifadhiwa) aliyeunda kikundi hewa cha watu watano na kuomba mkopo wa Sh. milioni tano kwa kushirikiana na ofisa maendeleo ya jamii, baada ya kuzipata aliwapatia wajumbe wake kila mmoja Sh. 100,000 na yeye kubaki na Sh.milioni 4.1.

Alisema fedha hizo alizitumia kununua pawatila la kilimo ambalo nalo halikuweza kudumu na kuharibika na mwisho wake liliibiwa na watu wasiofahamika na hakuweza kuurejesha mkopo huo mpaka pale ofisa maendeleo alipohamishwa kituo cha kazi.

Macha alisema ofisa maendeleo mpya alianza kufuatilia kikundi hicho kutokana na kutokurudisha fedha hizo na kubaini hujuma hizo zilizofanywa na diwani.

"Tulimwita diwani tukamhoji na akakiri kuchukua fedha na sasa amekubali kuzilipa fedha zote na anaendelea na marejesho yake,"alisisitiza Macha.

Ofisa Maendeleo wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Robert Kwela alisema kwa sasa hana vikundi hewa na badala yake wale wanaoshindwa kulipa kwa muda viongozi wao wanafikishwa mahakamani.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa msingi wa madarasa ya sekondari mpya ya Kisiwa cha Rubuka, jimbo la Musoma Vijijini, mkoani Mara jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wananchi Nyatwali kupisha upanuzi hifadhi ya Serengeti

**Na Vitus Audax,** MARA

WANANCHI wa Kata ya Nyatwali wilayani Bunda mkoani Mara wametakiwa kuhama haraka katika maeneo hayo ili kupisha upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti (SENEPA).

Agizo hilo lilitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi wakati wa mkutano wa hadhara na wananchi wa Mji wa Bunda uliofanyika katika uwanja wa stendi ya zamani na kuwahakikishia kulipwa fidia kuanzia wiki ijayo.

Mtambi alisema malipo yapo tayari na kuwataka wananchi kujiandaa kupokea fidia zao kutoka Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) na kuhama katika eneo hilo.

Aidha, aliwataka Wakurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda na Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kuhakikisha wanaitisha vikao vya baraza la madiwani kujadili na kutenga maeneo maalum ya kuwauzia wananchi watakaohama kutoka katika Kata ya Nyatwali kwa bei nafuu ili kuwasaidia watakaotaka kubaki ndani ya Wilaya ya Bunda kupata maeneo kwa haraka.

Mkazi wa Kata ya Nyatwali, Peter Chacha alisema wanaishi kwa wasiwasi katika eneo hilo kutokana na kwamba hawajalipwa fidia, na kwamba wakilipwa wako tayari kuhama.

# Mganga Mkuu ataka agenda ulinzi, usalama wa mtoto ipewe kipaumbele

**Na Restuta Damian,** KAGERA

MGANGA Mkuu wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Kagera Bukoba, Dk. Samwel Laizer amesema ni wakati wa jamii kuweka kipaumbele kwenye agenda ya ulinzi na usalama wa mtoto badala ya kuacha jukumu hilo kwa wataalam pekee.

Aidha,ikiwa kila upande utatimiza wajibu wake kitakuwa kizazi chenye afya bora na tabia njema.

Dk. Laizer alitoa kauli hiyo juzi wakati wa ufunguzi wa kikao cha robo ya tatu ya mwaka cha program jumuishi ya malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto, inayotekelezwa na halmashauri za mkoani hapa ili kuwezesha ustawi bora wa watoto nchini.

Alisema pamoja na mafundisho yanayoendelea kutolewa shuleni, jamii inapaswa kutoa elimu ya ulinzi na usalama wa watoto ikiwamo kuwafundisha kujitambua na kufahamu nafasi yao, jinsia na wasiharibiwe na tamaduni za kigeni kama ushoga na usagaji.

Kwa mujibu wa Dk. Laizer, mtoto huanza kujengewa uelewa katika katika hatua ya malezi na makuzi kati ya umri sifuri kuendelea, ili anapofikia utu uzima ajitambue kutenda na kutambua mazuri na mabaya kwa jamii.

Mratibu wa progamu hiyo mkoa, Issa Mrimi alisema program hiyo inawalenga watoto wa umri wa miaka sifuri kuendelea, kwa lengo la kuhakikisha wanakuwa vyema kwa ajili ya kupata kizazi chenye maadili na afya njema.

"Bado utekelezaji wa program hii unaoendelea hadi 2026 ni lazima sasa kuwa na malengo yatakayoonesha mafanikio katika kumhudumia mtoto kwa kuwa serikali imejielekeza kwenye ustawi wa mtoto na uwepo wake,"alisema Mrimi.

Ofisa ustawi wa jamii Wilaya ya Ngara, Mussa Barangodoza alisema katika utekelezaji wa program hiyo wamebaini idadi kubwa ya wazazi wamejikita zaidi katika utafutaji na kusahau jukumu lao la malezi.

## Elimu dawa za kulevya kuhamishiwa shuleni

**Na Vitus Audax,** MWANZA

SERIKALI imesema ili kudhibiti kikamilifu matumizi ya dawa za kulevya nchini, imeweka utaratibu wa kutoa elimu kama inayotolewa kwa umma katika shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu kama ambavyo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wanafanya.

Kauli hiyo imetolewa juzi jijini Mwanza na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa katika kilele cha maadhimisho ya kitaifa ya kupiga vita dawa za kulevya duniani ambayo yalifanyika katika Uwanja wa Nyamagana.

"Ni lazima tuimarishe mikakati yetu ya kukabiliana na mapambano haya na serikali imejikita katika kutoa elimu ili jamii ifahamu, na tutakwenda kuanzisha klabu katika shule za msingi, sekondari hadi vyuo vikuu kama walivyofanya TAKUKURU ili kupunguza kama si kumaliza kabisa tatizo hili," alisema Majaliwa

Aidha, aliwataka vijana wa kitanzania kuachana na matumizi na biashara ya dawa za kulevya na badala yake waungane kufanya shughuli halali za kiuchumi, ili wajiletee maendeleo katika ngazi ya familia, jamii na hata Taifa.

Alisema jamii inatakiwa kuelimishwa zaidi kuhusu athari za matumizi ya dawa hizo na kuwa njia hiyo itakuwa mwarobaini wa tatizo hilo sugu pamoja na kuwawezesha waliotoka kwenye uraibu (waraibu) kujumuika na wenzao kufanya kazi na kujisimamia.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda akitoa taarifa ya hali ya dawa za kulevya katika Mkoa wa Mwanza kuanzia mwaka 2018 hadi 2023, alisema wananchi waliopatikana na bangi ni 1,797, mirungi 294, dawa za kulevya (cocaine, heroin na nyingine) 51 na kufanya jumla ya dawa zote kuwa 2,142.

"Takwimu hizi zinabainisha kwamba biashara na matumizi ya dawa za kulevya hapa Mkoani Mwanza ni kubwa na inahitaji msukumo mkubwa kutoka kwa serikali pamoja na wadau mbalimbali, ili kuendelea kupambana na wazalishaji, wasambaji na watumiaji wa dawa hizi,"alisema Mtanda.

Wahitaji Zanzibar waelekea kuwa mfano wa kuigwa kimafanikio kijamii, kiuchumi

Ukurasa 13






Ukurasa 14

VIJANA WANAHITAJI HAYA KUKIPENDA KILIMO

**Ubunifu, uwekezaji kwenye zana za kisasa matrekta yanayolima, kupanda, kusindika.....**



TEKNOLOJIA
NA GAUDENSIA MNGUMI

DK NEVER MWAMBELA

# Mgunduzi dawa isiyo na kemikali, kutibu mazao

• Inazalishwa Tanzania kusambazwa Afrika

BAADA ya kuhitimu shahada ya uzamivu katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela-Arusha, Dk. Never Mwambela, anaandika historia Tanzania na Afrika pia.

Ni ya ugunduzi wa kwanza unaofanywa na mwanamke Tanzania na Afrika, akibuni kiuatilifu hai kisicho cha kemikali kinachotumika kudhibiti visumbufu kama kantangaze kwenye nyanya, viwavijeshi vinavyoharibu mahindi na viwavi vitumba jamii ya wadudu waharibifu kwenye pamba.

Amefanya shahada ya uzamivu (PhD) kwenye kantangaze na kugundua kiutilifu kinachoitwa 'Vuruga Biocide.' Ni kiuatilifu hai (hakina sumu wala kemikali), lakini hakuishia hapo ameanzisha kampuni ya Plant Biodefenders mwaka 2019 na kusajili kiuatilifu hicho kinachotumika nchini na juhudi za kukisambaza Afrika zikiendelea.

**KANTANGAZE NININI?**

Mtafiti huyu anapozungumza na Nipashe, anaeleza kuwa kantangaze' ni wadudu vamizi waliotokea Amerika ya Kusini tangu mwaka 1914 na kusambaa Ulaya miaka ya 2000 na hatimaye Tanzania 2014 wakionekana kwanza eneo la Ngarenanyuki mkoani Arusha na sehemu nyinginezo.

"Ni mdudu mdogo sana lakini ana athari kubwa anashambulia hatua zote za mmea kuanzia miche, majani, shina, maua na matunda ya mazao jamii ya nyanya ikiwamo nyanya zenyewe, pilipili hoho, nyanya chaungua na mboga ukiwamo mnavu"



Nyanya iliyoshambuliwa na kisumbufu kantangaze.

Pia anaharibu pipipili zote, biringanya na magugu yenye jamii ya nyanya kama ndulele hivyo kusambaa kwa haraka hasa wakati wa kiangazi na joto." Anaongeza.

Anasema PhD yake, imefanyika kwenye vivamizi hivyo ambavyo hushambulia kwa kasi mahindi na kwamba, alianza kukizalisha kiutalifu cha kupambana na mdudu huyo katika maabara ndogo iliyotengeneza lita 100 za dawa kwa wiki wakati wa usajili mwaka 2020.

Mhadhiri huyu mwandamizi na Meneja wa Taaluma wa Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Afrika-Mweka, mkoani Kilimanjaro, pia ni Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Plant Biodefenders, anayoimiliki.



Mbunifu wa kiuatilifu vuruga Dk.Never Mwambela. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

Akizungumzia mafanikio ya ubunifu wake anasema:"Kwasasa kampuni imejenga kiwanda chenye thamani ya Sh.milioni 680 na imeajiri wafanyakazi 12 wa kudumu na watatu wa mkataba na ajira za muda mfupi na vibarua 20 pia wapo."

Anaeleza kuwa kiwanda hicho kipo Shirimatunda mkoani Kilimanjaro, na kwamba ujenzi hadi Disemba 2023 uligharamu Sh 680,000,000 na wadau kadhaa wanahusika na uwekezaji huo.

Anawataja kuwa ni pamoja na yeye mwekezaji na mdau mkuu, wanahisa, serikali, Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), UDPF-UNCDF, KFW-DeveloPPP ( ya Ujerumani) kupitia Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU).

"Tumetengeneza ajira nyingine pia kupitia mawakala wa viuatilifu katika mikoa mbalimbali na tunaendelea kuajiri vijana wengi na wanawake kwa kuwa kiuatilifu hakina athari za kiafya hivyo kuwavutia vijana zaidi." Anaongeza:

Aidha, anasema kiwanda kina uwezo wa kuzalisha lita 1,000 za kiuatilifu hai kwa siku zinazoweza kunyunyiziwa kwenye heka 8,000 za mashamba kwa siku, hivyo kutoa mchango mkubwa wa kupunguza tatizo la upungufu wa viuatilifu pia matumizi ya kemikali za sumu zinaoathiri ikolojia.

Anasema :"Pamoja na hayo hiki ni kiwanda cha kwanza na cha kipekee nchini na Afrika kwenye kutengeneza viuatilifu hai. Kimesajiliwa kina haki miliki namba Africa Regional patent No. AP/P/2019/01149. Kinatambulikwa kuwa kinachozalisha kiuatilifu chenye ufanisi katika maeneo matatu kwa wakati mmoja."

**UFANISI WA VURUGA**

Anaeleza kuwa ni kuua visumbufu kwa asilimia 80 mpaka 100,

INAENDELEA UK.12

# Mgunduzi dawa isiyo na kemikali, kutibu mazao

INATOKA UK.11

kurutubisha mimea, kupunguza matumizi ya mbolea na huvutia wadudu rafiki kama nyuki ili kuongeza uchavushaji na mavuno pia huku kikipunguza gharama za uzalishaji.

Anasema :"Kwasasa kampuni imewafikia wakulima zaidi ya 9,000 pekee japo idadi ni kubwa zaidi. Kimeokoa zaidi ya eka 72,000 za mazao kwa mwaka ambao ni wateja wa kudumu wanaolima mahindi, nyanya na pamba."

Dk. Never anasema kwenye mahindi vuruga imenusuru heka 3,200, nyanya 4,000, pamba 4,500, mboga na parachichi heka 300 katika mikoa ya Simiyu, Shinyanga, Kilimanjaro, Tanga, Mwanza, Arusha, Morogoro, Tabora, Pwani, Dar es salaam, Iringa, Njombe, Unguja, Zanzibar, Mbeya na Manyara.

Pamoja na mafanikio hayo, baada ya kujenga kiwanda hicho anasema kampuni yake imepunguza bei za kiuatilifu kwa asilimia 10 ili kuwawezesha wakulima kumudu zaidi na kuepuka hasara hasa kwenye mahindi ambako viwavi jeshi vamizi vinaleta uharibifu mkubwa na kusababisha upotevu wa chakula pamoja na hasara kwa mkulima.

Anasema:" Pia kampuni ipo katika hatua za kusajili viuatilifu vingine hai na mbolea za asili ili kuleta tija katika sekta ya kilimo na kupunguza matumizi ya kemikali ambazo zinaathiri bayoanuai na kutishia afya za wanadamu."

Mtaalamu huyu , anasema kutokana na kiwanda hicho kuhudumia sekta ya kilimo ambayo ina umuhimu wa kipekee kwenye kufikia utoshelevu na usalama wa chakula, kinakusudia kuleta mabadiliko ya kilimo hai na kuongeza tija katika uchumi endelevu kwa kuwalenga vijana na wanawake.

Anaongeza kuwa vuruga haina kemikali wala kiambata sumu, na imetengenezwa kwa kiambata hai fangasi aina ya 'A.oryzae' ndicho kinachoua wadudu na kuboresha udongo na mimea.

Kadhalika,haileti usugu kwa wadudu kwakuwa hakuna kiambata kemikali (chemical active ingredient).

"Kiuatilifu hiki kina mchango mkubwa kwenye ikolojia kwakuwa ni fangasi ambayo inarudisha vimelea na virutubisho kwenye udongo na haina athari kwa viumbe wasiokusudiwa kama nyuki.

Pia tumefanya majaribiao kwenye pamba mfano mbegu za Afrisian mkoani Simiyu na Shinyanga, kahawa-KPL mkoani Kilimanjaro na mahindi Kibaha mkoani Pwani."

Anasema taasisi ya Biocontrol inayohusika na kufuatilia na kutafiti matumizi ya viumbe hai kama fangasi, mimea na wadudu, ina ushahidi wa kitafiti uliochapishwa na kuonyesha kuwa vuruga inavutia nyuki na wadudu wengine kama buibui wenye kazi kubwa kwenye ikolojia.

" Ikutumiwa kwenye nyanya zinazaa sana na kutoa maua mengi na kuvunwa mara nyingi. Katika mahindi yakikatwa kiini na kiwavijeshi 'Vuruga Biocide' ni tiba kwakuwa ina kiambata cha kimelea cha asili , kinawezesha kuchipusha upya na mimea ya jamii ya matunda ya miti mfano maembe, machungwa, mapapai yaliyojeruhiwa huchipuka kwa kasi pia.Yote haya tumetafiti na tuna majibu ya kiutafiti."



Mahindi yaliyoshambuliwa na viwavi vamizi ambavyo huharibu majani, shina, mhindi, gunzi na kusababisha uharibifu mkubwa.. **PICHA: MTANDAO**



> Mbolea asili zitasajiliwa ili kuzalishwa baada ya utafiti, ambazo anasema zinashika kasi na zitatatua changamoto inayotokana na chumvichumi kuharibu ardhi na kuathiri walaji.

Wakulima wengi wanaguswa na suala la bei , anapoulizwa gharama ya kiuatilifu hicho, anasema kuwa lita moja inauzwa Sh.30,000 na ina uwezo wa kunyunyiziwa kwenye eneo lenye ukubwa wa zaidi ya heka sita.

Anasema kuwa wakulima wakinunua watapata maelezo zaidi ya matumizi kwa wauzaji na pia vipeperushi vitawapa uelewa zaidi .

### KUTIKISA AFRIKA

Dk. Never anasema yeye ni mtoto wa Afrika, japo anaanza kwanza kazi nyumbani lakini ana mpango wa kusambaza vuruga kwenye mataifa mengine ya Afrika ili kudhibiti wadudu jamii ya kantangaze.

Anasema visumbufu hivyo vinavyofahamika kitaalamu kama (Tuta absoluta) na viwavijeshi vamizi (fall armyworm) na viwavi wa vitumba vya pamba (boll worm), wadudu wa parachichi (False codling moth) wapo maeneo mengi ukanda wa Afrika na kwa karne nyingi hawajapata suluhisho.

"Wadudu hawa wamesababisha usugu kwenye viatilifu vya kemikali na kuacha mabaki ya kemikali za sumu kwenye mazao na kukwamisha soko la nje hasa kwenye parachichi. Vuruga biocide ina ufanisi na haiachi mabaki, wala kemikali kwenye chakula hivyo ni salama kwa mlaji na mazingira.

Anaongeza kuwa wakulima wa pamba wanaoitumia wanasafririsha pamba yao Japan, German na China bila vikwazo kwakuwa haina mabaki ya sumu.

### MBOLEA ZIKO NJIANI

Akizungumzia mbolea za asili, anakiri zipo nchini kutoka kwa wajasiliamali wengi, hivyo kampuni ya Plant Biodefenders itaongeza nguvu na kwamba wanakuja kusajili aina nyingine.

Anasema mbolea asili zitasajiliwa ili kuzalishwa baada ya utafiti, ambazo anasema zinashika kasi na zitatatua changamoto inayotokana na chumvichumi kuharibu ardhi na kuathiri walaji.

Anasema kwa sasa mbolea za mwani au mazao ya bahari ndiyo tegemeo: "Mbolea inayotokana na mwani ndilo suluhisho la kudumu kwakuwa kilimo cha mwani ni chachu endelevu ukanda wa pwani ya Tanga na Pemba."

Anafafanua kuwa kila bidhaa zilizotengenezwa zimetafitiwa, zina haki miliki na hadi sasa ana haki miliki nne za mbolea na zina tuzo za kimataifa na kitaifa.

Dk. Never kuanzia mwaka 2020 ni mhadhiri mwandamizi na Meneja wa Taaluma katika Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Afrika cha Mweka, akishughulikia kupanga na kuratibu miradi ya ubunifu inayoboresha maisha ya watu.

Kadhalika, anasimamia na kuendeleza uhifadhi wa bayoanuai na teknolojia zinazotunza mazingira kwa uendelevu.

ELIMU

NA RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR

# Wahitaji Zanzibar waelekea kuwa mfano wa kuigwa kimafanikio kijamii, kiuchumi

TANZANIA imesaini na kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu unaozitaka nchi wanachama kuondoa ubaguzi kwa misingi ya ulemavu maeneo ya ajira.

Mkataba unaeleza kuwa wenye ulemavu wana haki ya kufanya kazi sawa na watu wengine.

Licha ya hatua mbalimbali kuchukuliwa kulinda wanaoishi na ulemavu, kama kutunga sheria ya watu wenye ulemavu na kuwawezesha kwa mikopo ya halmashauri changamoto zinaendelea kuwakabili na wana vikwazo vingi mbele yao.

Vikwazo hivyo ni hali ngumu ya maisha, kukosa mitaji ya kufanya biashara, kukosa elimu ya ujasiriamali na kukosa mikopo dhana ambayo sio sahihi ya kwamba hawakopesheki.

Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) - Zanzibar kwa kushirikiana na shirikisho la Watu Wenyeulemavu Zanzibar (SHIJIWAZA), wanaleta ukombozi kwa kundi la wenye mahitaji maalumu.

Wanashirikiana kwenye mradi wa Kijaluba, unaowakusanya wenyeulemavu na kuwapa elimu ya ujasiriamali ili kuachana na hali ya utegemezi.

Mratibu wa Kijaluba Khairat Haji, anasema baada ya kuwapa elimu ya ujasiriamali waliwashajihisha kuunda vikundi vya kuweka na kukopa ili kujipatia kipato cha kuendesha maisha yao na kuweza kujitegemea.

Aidha, hatua ya kuamua kuvisaidia vikundi hivyo ni kuunga mkono mikakati ya serikali katika kuwawezesha wananchi kiuchumi pamoja na kuwapatia mitaji ya kuanzisha miradi mbalimbali ya kimaendeleo.

Khairat anawataka viongozi na wanachama wa vikundi hivyo, kuyafanyia kazi maelekezo ya kitaalamu wanayopewa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kuanzishwa kwa vikundi hivyo.

"Hivi sasa tunakamilisha mwaka mmoja tangu mradi huo kuanza kuwasaidia watu wenye ulemavu na kuwafundisha kujua haki zao, elimu ya kuweka na kukopa, umuhimu wa kuweka akiba, kutengeneza sabuni, mikoba, ukulima wa mboga na biashara ndogondogo," anasema.

Lengo limefikiwa kwa sababu mwanzo ilikuwa ni ngumu kutokana na jamii kuwa na mitazamo hasi ya kwamba watu wenye ulemavu ni wa kupewa badala ya kutafuta, lakini wamehamasika kufanya biashara na kuanzisha vikundi vya kuweka na kukopa, anasema.



Wanavikundi vya watu wenye ulemavu vya kuweka na kukopa wakiwa katika vikao vinavyofanyika kila wiki. **PICHA:RAHMA SULEIMAN**

Aidha, anaeleza kuwa wanufaika wamejengewa uwezo wa kujua, umuhimu wa kuweka akiba, jinsi ya kutumia mikopo, elimu ya biashara na mbinu za kuendesha biashara kulingana na hali zao.

"Tumetoa mafunzo mbalimbali kujua haki zao, umuhimu wa kuweka na kukopa na jinsi ya kutumia mikopo na kufanya biashara na kuziendesha,"anaeleza Khayrat Haji, Ofisa Msaidizi wa Mradi wa Kijaluba.

Anaongeza, "Lengo kuu la mradi limefanikiwa kwa sababu haikuwa rahisi kubadilisha mitazamo iliyojengeka katika jamii kwamba wenye ulemavu ni wa kupokea zaidi misaada badala ya kujishughulisha na kujiongezea kipato".

Ofisa mwezeshaji wa vikundi vya kijaluba Muhidin Ramadhani, anasema wameweka utaratibu wa kukutana na wanavikundi hao kila muda ili kubadilisha mawazo na kubaini matatizo yaliyopo na kuyatafutia ufumbuzi wa haraka.

Anasema wenye ulemavu wakiwezeshwa wanaweza kwa sababu mradi huo umepelekea kuimarika kwa watu wenye ulemavu na kupiga hatua kimaendeleo na kufikia malengo ya kujikwamua na tatizo la umasikini.

Muhidin anasema mradi unaendelea na kuvisajili vikundi vilivyopo chini ya mradi huo kupitia Idara ya Ushirika ili vitambulike kisheria.

"Lengo la kuvisajili ni kupata fursa ya kufungua akaunti benki na kutunza fedha katika mazingira bora na salama," anaeleza Muhidin.

Ramadhani Haji, Mwenyekiti wa Kikundi cha Ushirika Tutambuwane kutoka kijiji cha Bwejuu Kusini Unguja, anaeleza kuwepo mradi umewasaidia watu wenye ulemavu kutatua baadhi ya changamoto zinazowakabili wao wenyewe ikiwa ni pamoja na kusomesha watoto na kuhudumia matibabu ya wagonjwa.

"Kupitia mfuko wa jamii, fedha zetu tunazoweka tumetatua matatizo mbalimbali. Tulipata maafa baadhi ya nyumba zetu kuingia maji na tukapata mkopo, pia wagonjwa waliolazwa walifaidika na mkopo huo kupitia jamaa zao waliojiunga kwenye vikundi," alisema.

> Tumetoa mafunzo mbalimbali kujua haki zao, umuhimu wa kuweka na kukopa na jinsi ya kutumia mikopo na kufanya biashara na kuziendesha.

Anafahamisha kwamba mradi umeandaa mwongozo maalum wa utekelezaji katika kusimamia uendeshaji wa vikundi vya hisa kwa lengo la kuongeza ujumuishaji wa watu wenye ulemavu katika shughuli za kiuchumi kwenye jamii.

"Ili kuongeza ujumuishi unaolenga kuwawezesha wenye ulemavu kiuchumi, mradi umeandaa mwongozo unaweka mazingira rafiki ya kukuza uwezo wa watu wenye ulemavu kiuchumi kwa kujenga mitazamo chanya juu ya ushiriki wao na kujiingiza katika shughuli za kujipatia kipato kupitia vikundi vya kuweka na kukopa," anasema.

Anasema ili malengo hayo yafikiwe ni lazima walimu na wawakilishi wa jumuiya za watu wenye ulemavu kutumia mwongozo kusimamia na kuwaelimisha watu hao umuhimu wa ushiriki wao katika shughuli za kujipatia kipato bila kujali hali za ulemavu wao.

Fatma Abrahman mwalimu wa vikundi anawataka walimu kushughulikia changamoto za wenye ulemavu bila kukata tamaa kulingana na hali za ulemavu ili kusaidia kujenga mitazamo chanya ya ushiriki wao katika shughuli za kiuchumi.

"Walimu wa vikundi tunatakiwa tusikubali kushindwa na kukata tamaa katika kuwasimamia watu wenye ulemavu. Tuwaongoze kutokana na uhalisia na utaalamu wetu ili tuwasaidie kufikia maelengo na kuwawezesha watu kiuchumi kupitia vikundi vya hisa," Fatma Abrahman.

Asha Haji Awesu, katibu wa kikundi cha mwanzo mgumu cha watu wenyeulemavu katika Kijiji cha Michamvi, mkoa wa Kusini Unguja, anasema wamefarajika kuanzishwa kwa vikundi hivyo kwasababu vimewasadia kupata mahitaji muhimu ikiwemo kulipia ada za shule kwa watoto wao.

Alisema mradi wa kijaluba umewapatia elimu ya ujasiriamali unaowawesha kuibua miradi mbalimbali ikiwamo kutengeneza sabuni, achari na vipodozi na mafuta.

Aidha anasema changamoto kubwa inayowakabili ni ukosefu wa mikopo kwa taasisi zinazotoa mikopo zikiwamo benki pamoja na soka la uhakika la kuuza bidhaa.

ELIMU
NA MAULID MMBAGA

### VIJANA WANAHITAJI HAYA KUKIPENDA KILIMO

# Ubunifu, uwekezaji kwenye zana za kisasa matrekta yanayolima, kupanda, kusindika

UWEKEZAJI kwenye zana za kisasa kuanzia matrekta, mbegu bora na miundombinu ya kilimo isiyotegemea mvua wala kuathiriwa na ukame ndiyo njia ya kuwaondoa vijana kwenye chuki dhidi ya kilimo.

Ni maoni ya wadau wa kilimo, wanaoeleza kuwa mapinduzi ya kilimo hayatokani na kingine bali zana bora, mbegu na matumizi ya teknolojia shambani ili kuongeza mnyororo.

Wanataja zana hizo kuwa ni pamoja na matrekta makubwa kwa madogo ya kulima, kupanda, kupalilia, kunyunyiza dawa, kuvuna na kuchakata zikipatikana zitawavuta vijana kupenda kilimo lakini, pia kukuza uchumi, kumaliza njaa na kukabiliana na uhaba wa ajira.

Akizungumza na Nipashe kwenye shamba darasa linaloandaliwa na Kituo ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Mikocheni Dar es Salaam, mkulima Gideon Mwendiumi, anasema zana za kisasa na teknolojia ni muhimu katika kurahisisha uzalishaji shambani.

Anasema Marekani, China, Russia, Ufaransa pamoja na Misri kwa upande wa Afrika zimepiga hatua kubwa katika sekta ya kilimo kutokana na kutumia vifaa vya kisasa kuzalisha mazao mbalimbali pamoja na mamilioni ya tani za vyakula kwa mwaka.

Mwendiumi meneja mstaafu wa kituo cha TARI, anaeleza kuwa ili kilimo kibaki uti wa mgongo na kutoa ajira kwa vijana, lazima serikali iweke mkakati wa kuwekeza vifaa vya kisasa na kuwapatia wakulima ili kuongeza kasi na tija ya uzalishaji, akisema vijana wengi wanakikimbia kutokana na ugumu wa kukiendesha.

"Wakulima wengi wanaona kama kilimo ni utumwa kwa sababu ya kutumia jembe la mkono. Mataifa makubwa yanatumia matrekta madogo kwa makubwa kulima maeneo makubwa kwa muda mfupi, kadhalika kuyahudumia na kupata tija kwa wepesi na kwa ufanisi.

"Tukiwekeza katika zana za kisasa vijana hawatakata tamaa, kumekuwa na malalamiko kwamba wengi wanakimbilia mjini, ni kwa sababu wameona wazee wanapinda mgongo ni shida ya kushika jembe, wakaona hii kazi hatuiwezi twende mijini. Wapo wanafanya kazi za ovyo, nia yao wapate fedha, hivyo tukiboresha wengi watalima," anashauri Mwendiumi.




Mkulima wa minazi Gideon Mwendiumi, anayemiliki zaidi ya ekari 11 za zao hilo wilayani Mkuranga, akitoa maelezo ya namna bora ya kulima nazi kwa tija. **PICHA: MAULID MMBAGA**

> "Nazi ni muhimu kwasababu zinahitajika katika chakula na kutengeneza thamani mbalimbali ambazo zina soko kubwa linalotoa fursa za ajira ndani na nje ya nchi.

### ALILIA MINAZI

Mwendiumi, mkulima wa nazi wilayani Mkuranga mkoa wa Pwani, anasema kilimo hicho kinawasaidia wengi kwasababu upatikanaji wa nazi nchini ni mdogo ikilinganishwa na mahitaji, akieleza kuwa matumizi ya bidhaa hiyo pamoja na mafuta yake bado ni makubwa licha ya kilimo chake kuwa chini.

"Kilimo cha minazi kinashuka kwa sababu nyingi, mfano Mkuranga wilaya inayoongoza kwa viwanda vingi, ujenzi wake umesababisha minazi mingi kukatwa na hakuna juhudi za kupanda.

"Hali hiyo inasababisha upungufu wa nazi kwenye soko kuwa mkubwa, nimeona huko mtaani wengi wameanza kuhamasika kutaka kupanda minazi baada ya kuona moja inafika mpaka 1,000. Wanasema kumbe inaweza ikawa sehemu ya ukombozi.

"Lakini kilimo cha mnazi ni kigumu, ugumu wake uko kwenye mambo matatu magonjwa, wadudu na maandalizi ya kuhakikisha zao linakuwa katika maeneo yanayouzika, kwa sababu elimu ya upandaji ni ile iliyozoeleka na mababu zetu toka miaka hiyo."

Anataka elimu itolewe sambamba na kuwekeza katika teknolojia ili watu walime kwa urahisi huku wakiwa na uelewa, ndiyo maana kituo cha TARI Mikocheni kinahamasisha watu kujua umuhimu wa kuchagua mbegu bora wakishirikiana na wataalamu ili kupunguza athari za magonjwa.

### MKAKATI KUINUSURU

Meneja wa kituo cha TARI Mikocheni Dk. Fred Tairo, anasema kuna mkakati wa kufufua kilimo cha nazi kwa kuendesha utafiti, kutenga ardhi na fedha kwa ajili ya kupatia vikundi vya vijana watakaokuwa na utayari wa kujihusisha na kilimo cha zao hilo.

Dk Tairo anaeleza kuwa baada ya vijana kupata mafunzo watapatiwa eneo, mbegu na fedha kwa ajili ya huduma za kilimo mpaka watakapofikia hatua za kuvuna mbegu na kuziuza, na kwamba fedha itakayopatikana watarudisha kiasi na nyingine wataitumia kujiendeleza.

"Kwa muda mrefu nazi imesahaulika kwa sababu mbalimbali na kusababisha kushuka uzalishaji lakini serikali imeamua kufufua kwa ajili ya kuongeza tija, ikiwemo pia kufufua mashamba mapya na kuendeleza ya zamani na kusambaza kwa wakulima takribani mbegu milioni 10 kwa mwaka.

"Changamoto inayowasibu vijana wengi hawana taarifa ya hizi za fursa ambazo zipo, ndiyo maana serikali imeamua kutenga fedha kwa ajili ya kuwashawishi vijana waingie kwenye hizo fursa kama njia ya ajira, mojawapo kuanzisha vitalu na kukamua mafuta, sisi tunavyowasiliana nao tunawapa elimu pana kwa mnyororo wa thamani wa zao la Nazi," anasema Dk. Tairo.

Vile vile, anaeleza kuwa wamekuwa na program ya kuwasaidia wakulima katika masuala mbalimbali ya kitaalamu, pamoja na kuongeza tija, huku akiwashauri kuachana na utaratibu wa kuziana nazi shambani badala yake wawe na utaratibu maalum ili kuongeza thamani.

"Nasisitiza katika suala la kuongeza thamani ya bidhaa hii kwasababu nazi ile ya kula nyumbani ambayo ataiuza kwa Sh 800 hadi 1,000 ndiyo inayotumika kutengeneza mafuta ambayo sokoni gharama yake itamnufaisha zaidi mkulima na kituoni kwetu tumeboresha mashine za kukamua na kuchuja mafuta.

Ofisa Kilimo Msaidizi Mkuu TARI Mikocheni, Violeth Kiwia, anasema nazi ni muhimu kwasababu zinahitajika katika chakula na kutengeneza thamani mbalimbali ambazo zina soko kubwa linalotoa fursa za ajira ndani na nje ya nchi.

Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga Khadija Ally, anasisitiza maofisa ugani kutoa majawabu ya changamoto zinazowakabili wakulima wakiwamo wanaojihusisha na nazi, na kuwafanya waone umuhimu wa kuweko kwa wataalamu hao katika kufanya kilimo endelevu na chenye tija katika maeneo yao.



## Wazawa wajitosa upanuzi TGC

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesaini mkataba wa bilioni 33.4 na kampuni mbili za wazawa kwa ajili ya upanuzi wa Kituo cha Gemolojia Tanzania (TGC) kilichopo mkoani Arusha kitakachotumika kutoa mafunzo ya uongezaji thamani madini nchini.

Kampuni hizo, Lumocons na Skyward za Kitanzania ziliingia mkataba huo na Wizara ya Madini juzi kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa jengo la ghorofa nane la kituo hicho kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo.

Akizungumza baada ya hafla ya utiaji saini jijini hapa, Naibu Waziri wa Madini, Dk. Stephen Kiruswa, alisema mradi huo unalenga kupanua kituo hicho ili kutoa mafunzo ya uongezaji thamani madini.

Kwa mujibu wa Kiruswa, Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, imeamua kuimarisha utoaji wa mafunzo katika kituo hicho kwa kupanua miundombinu, kuzalisha wataalamu wengi wa uongezaji thamani madini ya vito na madini.

"Serikali ya awamu ya sita imetoa Shilingi bilioni 33.4, shughuli za ujenzi zitaanza wakati wowote baada ya kusainiwa makubaliano leo (jana)," alisema.

Naibu Waziri huyo, alisema mradi huo ukikamilika utakiwezesha kituo hicho kutoa mafunzo kwa kiwango cha kimataifa na madini nchini yaliyochakatwa kupata soko la ndani na nje.

Alisema lengo la serikali kuanzisha kituo hicho ni kutekeleza Sera ya Madini ya Mwaka 1997 na kuongeza thamani ya madini nchini kwa kutoa mafunzo ya kuchonga miamba.

Kiruswa, alisema serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali katika uchimbaji madini na kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji nchini.

Alisema hatua zilizochukuliwa zimewezesha kuongezeka utafiti wa madini, uchimbaji madini, thamani ya madini na biashara zake, fursa za ajira na biashara kwa wananchi.

Akizungumzia kuhusu changamoto zilizopo katika sekta ya madini, alisema serikali inaendelea kutafuta wafadhili ili kupata mitaji kwa ajili ya uanzishaji wa viwanda vya kuchakata madini na maabara.

Mkurugenzi wa Lumocons', Andrew Shirima akizungumza kwa niaba ya kampuni hizo, aliishukuru serikali kwa kuwa na imani na kampuni za ndani ya nchini.

Shirima, alisema mradi huo utachochea ushindani miongoni mwa kampuni za ndani kutafuta zabuni kubwa za serikali.

"Kwa niaba ya washirika wetu wa utekelezaji, tunaahidi kutekeleza mradi kwa wakati na kwa weledi kama inavyotarajiwa na serikali," alisema.

# CCM 'yakunwa' ujenzi bweni alililogoma kuzindua RC

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida kimekipongeza Kiwanda cha Pamba cha Biosustain kilichopo Manispaa ya Singida kwa kufanikisha ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kike katika Shule ya Sekondari ya Mtekente iliyopo wilayani Iramba kwa gharama ya zaidi ya Sh.milioni 180.

Kiwanda hicho kimejenga bweni hilo lenye uwezo wa kupokea wanafunzi 80, jiko na kisima cha maji kwa fedha zake.

Katibu wa Siasa na Uenezi CCM wa Mkoa huo, Elphas Lwanji alitoa pongezi hizo juzi baada ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo kutembelea kiwanda hicho kinachomilikiwa na wazawa kwa lengo la kuangalia shughuli za uzalishaji zinavyofanyika.

Pongezi hizo zimekuja ikiwa ni takribani wiki tatu baada ya Mkuu wa Mkoa huo, Halima Dendego Juni 11, 2024 kukagua bweni lililojengwa katika sekondari hiyo na kugoma kuzindua kwa kile alichoeleza umaliziaji wake haukuwa mzuri.

"CCM inawapongeza Biosustain hapa Singida tumeona mnavyofanya kazi, mnatoa ajira kwa wananchi huko vijijini, mnawapa fedha za pamba kwa wakati wakulima na juzi juzi wamejenga mradi mkubwa wa bweni kwa ajili ya watoto wetu huko Iramba wa wafugaji na wakulima waweze kufikia malengo yao ya elimu," alisema.

Lwanji, alisema CCM imeridhika na namna kiwanda hicho kinavyofanya kazi katika sekta ya viwanda na ndio siri ya kuendeelea kuwepo kwa uzalishaji hadi sasa na kutoa ajira kwa wananchi wengi.

"Sisi kama CCM kwa niaba ya Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida, Martha Mlata, tunakupongeza Mkurugenzi kwa ushirikiano mkubwa unaotoa kwa chama, na mheshimiwa Waziri hawa (Biosustain) ni wadau wetu muhimu wakubwa kwenye chama chetu tunapokuwa na mambo ya kufanya wanatusaidia," alisema Lwanji.

Mkurugenzi Mkuu wa Kiwanda hicho, Sajjad Haider, alisema mwaka huu kimechukua mkopo wa takriban Dola za Marekani milioni 14 kwa ajili ya kuendeleza uzalishaji.

Prof. Mkumbo, alisema serikali inafurahishwa na uwekezaji unaofanyika katika kiwanda hicho kwa kuingiza fedha zinazokopwa kwenye mzunguko wa uchumi wa Mkoa wa Singida.

"Umuhimu wa viwanda ni kusaidia kuinua pato la Mkoa wa Singida, sasa nyie mnapokopa fedha sisi hilo ndio muhimu maana tunahesabu 'value' (thamani) ya kuingia kwenye uchumi wa mkoa wetu wa Singida," alisema.

Alisema serikali inahamasisha uchakataji wa mazao ya wakulima ya nafaka na biashara husasani pamba ambalo linalimwa katika mikoa 17 nchini.

"Karibu nusu ya idadi ya wakulima wanategemea zao la pamba, lakini changamoto iliyopo ni kwamba asilimia 80 ya pamba inayozalishwa Tanzania inauzwa kama malighafi kabla haijachakatwa," alisema.

Alisema nia ya Rais Samia Suluhu Hassan na serikali ni kouna uuchakataji wa pamba unafikia kiwango cha kati na kukitaka Biosustain kiwe mfano ili zao hilo lisiwe linauzwa kama malighafi na kuondoa na tatizo la wananchi kukosa ajira.

"Serikali itatoa kila aina ya ushirikiano ili kupunguza usafirishaji wa pamba nje ya nchi ikiwa katika hali ya ambayo ni ghafi, kuchakata nchini kuna uwezekano mkubwa wa kuzalisha ajira nyingi," alisisitiza Mkumbo.

Alisema serikali ipo katika hatua za kushughulikia changamoto za mashine za kielektroniki za kutoa stakabadhi (EFD) na kupitia upya mfumo wa kodi nchini.



Kaimu Msajili wa Jumuiya wa Wizara ya Mambo ya Ndani, Thomas Sanira akizungumza na Maaskofu na waumini wa kanisa la Free Anglican Church of Tanzania, wakati wa ibada ya kuwaweka wakfu maaskofu wa Dayosisi watano, iliyofanyika katika Kanisa la Mtakatifu Simon Petro Ushariki wa Ilazo, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# 340 wakatiwa bima ya afya, majanga

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MAKAMU Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino mkoani hapa, Kenneth Yindi, amewakatia bima wakazi 340 wa Kata ya Buigiri za afya na majanga.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati akikabidhi msaada huo kwa walengwa hafla iliyofanyika Kijiji cha Buigiri wilayani Chamwino, Yindi, aliwataja wanufaika hao kuwa ni pamoja na waendesha bodaboda 160, mabalozi 65, viongozi wa dini 40 na wajumbe wa serikali za vijiji vya Chinangali II Buigiri na Mwegamile wapatao 75.

Alisema bima hizo ambazo kazi yake ni fao la maisha ya mwanachama, pia zitawanufaisha walengwa hao kwa kutibiwa mume na mke, ulemavu uliotokana na majanga na wategemezi wanne ndani ya familia kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Aliwataka wanufaika hao kuzitumia bima hizo kwa malengo yaliyokusudiwa ili waweze kupata matibabu kupitia hospitali na vituo vya afya na zahanati zilizopo nchini.

"Ni matumaini yangu nyinyi walengwa mliopatiwa bima hizo za afya na majanga mtazitumia kwa malengo ili muweze kutibiwa kama mlivyoelekezwa," alisema.

Aliwaomba wadau wengine wa maendeleo kuwafikia watu waishio vijijini ambako bado kuna uhitaji mkubwa wa bima za afya ili kuwapunguzia gharama za matibabu.





# Wasiojulikana waiba kokoa mashambani, majumbani

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WATU wasiojulikana wanadaiwa kuvamia mashamba ya wakulima wa kokoa wilayani hapa Mkoa wa Mbeya, kuiba na kusababisha kupanda kwa bei ya zao hilo.

Bei ya zao hilo kwenye mnada wa mwisho ilipanda kutoka Sh. 6,000 kwa kilo moja mpaka Sh. 26,000.

Wimbi hilo la wizi wa kokoa linadaiwa kusababisha wakulima kulala mashambani usiku kulinda mazao yao yasiibiwe.

Vijiji vilivyopo Kata za Itunge na Ndandalo ni miongoni mwa maeneo ambayo wakulima wa zao hilo wamekumbwa na wizi huo.

Mmoja wa wakulima hao wa Itunge, Ambakisye Mwotela, alidai wezi hao baada ya kubaini wakulima wanalala mashambani, wamebadili mbinu kwa kuanza kuvamia majumbani mwao nyakati za usiku na kuiba kokoa.

"Hali hii imekuwa hatari kwetu kwa sababu tunalazimika kulala mashambani, wezi hawa wanaweza wakatudhuru ama tukang'atwa na nyoka, lakini kitendo cha wezi hawa kuanza kuja majumbani kinatutishia zaidi," alilalamika Mwotela.

Yesebia Kodi, alidai wizi wa zao hilo umekuwa mkubwa zaidi baada ya soko kuwa zuri kutokana na bei yake kupaa.

Kodi, alidai baadhi ya wezi hao wanachuma matunda mabichi, kuchemsha na kuchoma kwa moto na kuharibu ubora wa zao hilo.

"Hii yote ni kwa kuwa kipato ni cha juu, mtu anaona akipata lita mbili za kokoa anauza mpaka Sh. 30,000, tunaomba serikali itusaidie kutoa elimu maana michezo mingine kama hii inaharibu ubora wa zao letu," alidai.

Ibrahim Mohamed, alidai wezi hao wanapita mchana kwenye mashamba na kuweka alama kila tunda lililokomaa kisha kwenda kuiba usiku.

Alimuomba Mbunge wa Kyela, Ally Mlaghila kuwasaidia kuunda vikundi vya ulinzi shirikishi katika kata za jimbo hilo ili kudhibiti wizi huo.

Kwa upande wake, Kinanasi aliahidi kuwawezesha vifaa kwa ajili ya vikundi vya ulinzi shirikishi na kuonya watu hao kuacha wizi huo kwa kutafuta kazi nyingine halali ya kujiingizia kipato.

"Nimezungumza na polisi wa Kata ya Itunge, tumekubaliana kuanzisha klabu za ulinzi na walichoniomba ni vifaa kama makoti ya reflector, filimbi na tochi, ndani ya siku mbili nitatekeleza ili kazi ianze na wananchi msiibiwe tena," alisema Mlaghila

Alisema kakao kwa sasa inauzwa Sh. 26,000 kwa kilo na kwamba atahakikisha anafanya kila njia kukomesha wizi huo na uharibifu wa zao hilo..



Baadhi ya vijana wakazi wa Kijiji cha Chang'ombe, Kata ya Mjele, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wakisaidiana kushusha magunia ya mkaa kutoka kwenye pikipiki kwa ajili ya kuyauza, kijijini hapo, mwishoni mwa wiki iliyopita. Biashara hiyo imekuwa ikichangia uharibifu wa mazingira kutokana na ukataji wa miti inayotumika kutengeneza bidhaa hiyo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wanakijiji wafunzwa kutokomeza utapiamlo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Kijiji cha Inyala kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameanza kupatiwa elimu ya kukabiliana na udumavu kwa watoto kwa kukosa lishe bora.

Elimu hiyo inatolewa na Shirika lisilokuwa la kiserikali la ADP Mbozi kwa wananchi ya uandaaji wa chakula kwa watoto.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wa shirika hilo, Maneno Uledi, alisema elimu hiyo inalenga kuwasaidia wakulima kujua namna ya kuandaa lishe kwa watoto ili kupunguza kiwango cha udumavu katika wilaya hiyo.

Alisema pia wanaitoa elimu hiyo kwenye maeneo mengine ikiwemotaasisi za elimu ili kuhakikisha inasambaa kwa kasi zaidi.

"Tunashirikiana kwa kiwango kikubwa na serikali kutoa elimu hiii na lengo ni kupunguza tatizo hili la udumavu kwa watoto," alisema Uledi.

Ofisa Lishe wa Wilaya ya Mbeya, Namkundaelly Mmbaga, alilishukuru shirika hilo kwa kutoa elimu kwa wananchi hao na kutimiza malengo ya serikali ya kupunguza udumavu kwa watoto.

Mmbaga, alisema udumavu kwa watoto unasababisha matatizo mengine ikiwemo magonjwa, kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya chakula, na kiwango cha elimu.

"Sisi kama halmashauri tuna mikakati yetu ambayo tunatekeleza ya kupunguza udumavu, lakini huu utaratibu wenu mlioanzisha utatusaidia kufikia malengo yetu," alisema.

Aliwataka wananchi kuendelea kufuata ushauri wa wataalamu hao kuhakikisha watoto wao wanakua na afya njema.

**"Tunashirikiana kwa kiwango kikubwa na serikali kutoa elimu hiii na lengo ni kupunguza tatizo hili la udumavu kwa watoto," alisema Uledi.**

# Serikali yabisha hodi mikoa 14 kupinga ukatili wa kijinsia

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI imeanza kutekeleza muongozo wa uanzishwaji wa madawati ya kupinga ukatili wa kijinsia katika maeneo ya umma baada ya kuifikia mikoa 14 ili kukomesha vitendo hivyo nchini.

Mkurugenzi Msaidizi wa Masuala ya Jinsia kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Rennie Gondwe aliyasema hayo mkoani hapa wakati wa mafunzo ya waratibu wa madawati ya jinsia.

Gondwe, alisema kuwa wameanza katika masoko ambako ni miongoni mwa maeneo yenye mkusanyiko wa watu ambako vitendo hivyo kufanyika kwa kiwango kikubwa.

"Wizara imefanya mafunzo katika mikoa 13 na sasa tuko Njombe mkoa wa 14 ambako tunafundisha namna ya kuandaa dawati hilo, katika meneo ya umma hususani masoko," alisema Gondwe.

Alisema kupitia maofisa ustawi wa jamii, wananchi watapata uelewa juu ya dawati hilo ili wanapopata matatizo wajue kwa kupeleka malalamiko.

Mratibu wa Mpangokazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Linus Kahendaguze, alisema kuna ukatili wa aina mbalimbali unaofanyika maeneo ya umma dhidi ya wanawake na watoto.

"Moja tunafahamu kwa sasa wanawake wanajishughusha sana na shughuli za uchumi za uzalishaji kwenye maeneo mbalimbali yakiwepo masoko ambako kuna ukatili wa aina mbili," alisema Kahendaguze.

Alitaja moja kuwa ni lugha chafu dhidi ya wanawake zisizo na staha, hivyo kusababisha manung'uniko na kuathiri utendaji kazi wao.

Alisema nyingine ni wanawake kulazimishwa kujamiiana ili aweze kufanya biashara.

Ofisa Biashara Wilaya ya Ludewa, Hassan Sure, alisema maeneo ya umma hasa sokoni, stendi, kanisani, shuleni yamekithiri kwa a ukatili dhidi ya wanawake.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Njombe, Elice Simonile, alisema madawati hayo yatasaidia kubadili mienendo ya watu na kuheshimiana.





## Kongamano la kuvutia wawekezaji kufanyika nchini

**Na Mwandishi Wetu**

WATOA huduma za kifedha kwa njia ya mtandao kutoka nchi tano za Afrika wanatarajia kukutana nchini katika kongamano la wafanyabiashara Afrika Mashariki, ambalo litachochea ushirikiano katika uwekezaji.

Kongamano hilo liitwalo East Africa Investment Forum linatarajiwa kufanyika kwa siku mbili kuanzia Septemba 12-13 jijini Dar es Salaam na kuvuta wawekezaji mbalimbali.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa Chama cha Watoa Huduma za Kifedha kwa njia ya Mtandao (TAFINA), Cynthia Ponera, alisema kongamano hilo lina lengo la kuunganisha wafanyabiashara hususani watoa huduma za kifedha kwa njia ya mtandao kutoka nchi za Afrika Mashariki na Kati.

Alisema katika uandaaji wa kongamano hilo wamepata ushirikiano mkubwa kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ambao nao watashiriki.

"Tunafuraha sana kuandaa kongamano hili kubwa, lengo letu ni kuona wawekezaji na wadau tunaenda pamoja, kongamano hilo litachochea kwa kiasi kikubwa ushirikiano katika uwekezaji," alisema Cynthia kuongeza:

"Hapa nchini tunatarajia wanachama wetu, kampuni 62 zitashiriki, laikini pia tunatarajia washiriki kutoka nchi za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), tunaamini kongamano hili litasaidia kuwaleta wawekezaji watakaongalia fursa za uwekezaji hapa nchini," alisema Cynthia.

Alisema pia wataendelea kutumia kongamano hilo kuendelea kutoa elimu kwa wanachama wao namna ya kukabiliana na udanganyifu na wizi wa fedha kwenye mtandao.

Aidha, alisema taasisi na mashirika yatakayovutiwa kushiriki katika kongamano hilo watatakiwa kujiandikisha ili kupata uhakika wa kushiriki.

Mkuu wa Masoko wa Selecom, Shumbana Walwa, alisema kampuni hiyo ni mwanachama wa TAFINA na watahusika kukusanya ada za ushiriki kwa njia ya mtandao.

# Ushirikishaji vijana kunatatua matatizo yanayowasibu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MFUMO mzuri wa uratibu wa masuala ya vijana ni mkakati mojawapo ya kuwandaa vijana katika ushiriki na ushirikishwaji katika ngazi ya maamuzi kwa lengo la kutatua changamoto zao.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi inayopambana na changamoto za vijana Zanzibar (ZAFAYCO), Abdallah Abeid wakati akizungumza katika kongamano la vijana lililofanyika Zanzibar.

Abeid alisema ni muhimu kuwekwa mifumo rafiki ya kupata taarifa sahihi na kusambazwa kwa taarifa zinazohusiana na fursa za vijana ili wazitumie na kufaidika nazo.

Pia, alisema kongamano hilo limelenga kuwainua vijana kwa kuwatengenezea daraja la kushiriki katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kisiasa bila kuwepo kwa vikwazo vyovyote vitakavyochangia kurudisha nyuma jitihada zao.

"Kuwashirikisha vijana katika ngazi za maamuzi ni miongoni mwa njia ya kutengeneza viongozi sahihi wa baadae watakaoweza kuliongoza taifa lao," alisema.

Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi nafasi za vijana, Khuzaima Mbarouk alisema vijana wana haki ya kuchagua na kuchaguliwa, hivyo ni vyema kujitokeza katika kugombea nafasi za uongozi katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, ili kuongeza idadi ya vijana katika vyombo vya maamuzi.

Alisema ushiriki huo wa vijana utasaidia kupaza sauti zao katika vyombo sahihi vya maamuzi na kupitisha ajenda na sera zinazohusiana na vijana.

Hivyo, aliwataka vijana kushiriki katika mafunzo ya siasa na uongozi kwa sababu ni muhimu katika kutumia akili ya kuingia majimbo ya uongozi na sio kutumia nguvu.

Washiriki wa kongamano hilo akiwemo, Hija Abdalla alisema asilimia 50 ya vijana wanahusika katika nguvu kazi ya maendeleo, hivyo serikali inapaswa kuliangalia kwa jicho pana eneo hilo kwa sababu nao ni sehemu ya mchango katika nchi.

"Wadau wa vijana watengeneze mifumo rafiki itakayotusaidia katika kushirikishwa ndani ya majukwaa yote, ni vyema miongozo inayopitishwa vijana tupewe asilimia hasa katika uteuzi ikiwemo wakuu wa wilaya ili kuona mchango wetu," alisema Hija.

Mmoja wa wajumbe kutoka Taasisi ya Watu wenye Ulemavu Zanzibar, Asila Iddi alisema katika kongamano hilo amejifunza vijana kujitoa katika nyanja za uongozi na kufanya utafiti ili kupata maamuzi.

Kongamano hilo limeandaliwa na ZAFAYCO, PYI, CYD na KHF, kwa kushirikiana na NDI pamoja na USAID.



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Charles Kichere (kushoto), akipokea kitabu cha mwongozo wa mwanachama kutoka kwa Ofisa Mkuu wa Uhusiano wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Abdul Njaidi alipotembeela banda la mfuko huo, kwenye Maonyesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, kwenye viwanja vya Julius Nyerere Barabara ya Kilwa jana. Katikati ni Ofisa Huduma kwa Wateja wa mfuko huo, Nahira Mang'ana. **PICHA: MRAJI MSALA**

## Wanahabari watakiwa kufuata sheria, miongozo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Tume ya Utangazaji Zanzibar, Suleiman Ame Khamis amevitaka vyombo vya habari kufuata sheria na miongozo iliyowekwa na tume katika kuandaa na kuripoti habari kwa jamii.

Aliyasema hayo katika ufunguzi wa mafunzo kwa wadau wa habari kuhusu wajibu wa kuzingatia maudhui ya utangazaji na mwongozo wa kuripoti habari katika kipindi cha uchaguzi, yaliyofanyika katika ukumbi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar.

"Vyombo vya habari ndiyo tunavyovitegemea katika kuleta maendeleo ya nchi, hivyo basi nina imani kubwa mafunzo haya yatakuwa chachu ya kufanya mabadiliko chanya katika jamii na kudumisha amani ambayo ndiyo imetawala katika nchi yetu hasa katika kipindi tunachoenda cha uchaguzi" alisema.

Katibu Mtendaji wa Tume ya Utangazaji Zanzibar, Suleiman Abdullah Salim, alivitaka vyombo vya utangazaji kusajiliwa na kupatiwa leseni, ili kufanya kazi zake kihalali akisema kutofanya hivyo ni kufanya makosa na kwenda kinyume na sheria zilizowekwa.

Mrajis wa Tume ya Utangazaji, Mohammed Said Mohammed alisema vyombo vya habari wanaporusha maudhui wanapaswa kuzingatia staha na maudhui yanayoendana na mila na silka ya jamii.

Mrajis wa Idara Habari Maelezo, Jamila Mahmoud Juma aliwataka wamiliki wa vyombo vya habari kuhakikisha kabla ya waandishi wao kufanya kazi wahakikishe wamepatiwa vibali kutoka Idara ya Habari Maelezo.

## Serikali kumsaidia mkulima uzalishaji chakula

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imesema itaendelea kuchukua hatua katika kuimarisha sekta ya kilimo ili kumsaidia mkulima katika uzalishaji na upatikanaji wa uhakika wa chakula nchini uwe endelevu.

Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa uvunaji wa mpunga kwa wakulima na maofisa wa kilimo.

Alisema jitihada hizo zinaenda sambamba katika kuwainua wakulima hasa katika kuwajengea miundombinu imara katika shughuli za kilimo ili zitumike katika kuleta maendeleo makubwa na kujipatia kipato.

Alisema lengo la uzinduzi wa zoezi hilo ni kuona jitihada zinazoendelea kwa wakulima katika kilimo, kuzalisha chakula kwa wingi pamoja na kuhakikisha kilimo kinakua chenye tija.

Hata hivyo, alisema serikali ina nia njema katika kuwasaidia wakulima kwa kuingiza pembejeo ambapo zitachangiwa nusu kwa nusu na wakulima ili kuwapunguzia ugumu wa bei.

Shamata alisema kilimo cha mpunga endapo mkulima akiweza kusaidiwa na kuzikabili changamoto zao uzalishaji utaongezeka visiwani Zanzibar.

Naye Mratibu wa bonde hilo, Yussuf Faki Yussuf alimuomba Waziri huyo kuwasaidia katika punguzo la bei ya pembejeo, punguzo la umeme sambamba na benki mbalimbali ili waweze kuwapatia mikopo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**HILDA ELIAS MAHUNDI,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo chenye namba bea **0008672** kilichotolewa na chuo cha CBE Mwaka 2019, Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/27186/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GASPER B. MFOY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1880-0177** kilichotolewa na baraza la mitihani la taif kupitia shule ya sekondari ya MBEZI INN SECONDARY SCHOOL mwaka 2017,yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **PHQ/DAR/UBU/129051/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**TULIZAN .S. SALUM** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0822-0456** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia SINZA ITEBA mwaka 2007. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/131639/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**BASHIRU OMARI MKANE,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo chenye namba **REG/PWF/1001** kilichotolewa na chuo cha irdp Mipango Mwaka 2022. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/27203/2024**

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**

**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 14365 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the Late DAVID BENEDICT GERVAS**

**And**

**In the matter of Application for letters of administration by DATIVER JOSEPHAT MLAY**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters od administration) is made to the above named petitioner

Objections to the grant should be filed on or before the 24 day of 07 ..2024

Dated at DAR ES SALAAM this 21 day of 06 2024

TEMEKE DISTRICT COURT ONE STOP JUDICIAL CENTRE

Principal Resident Magistrate

## KUPOTELEWA NYARAKA UMILIKI WA KIWANJA

**ABDALAH ABASI ABDALAH**
anatangaza kupotelewa na Nyaraka ya Umiliki wa **Kiwanja namba 155 Kitalu "V"** kilichopo Ngokolo Manispaa ya Shinyanga Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Abdalah kwa simu namba 0652-922140.
TAARIFA YA POLISI :
**PHQ/SHI/SHI/5025/2024**

MUNICIPAL LAND OFFICER SHINYANGA

Lela Chipanyanga
AFISA ARDHI
MANISPAA YA SHINYANGA

## KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

**SAIMON JOEL KITANGENGI,** Anatangaza kupotea kwa ofa ya kiwanja **plot 51, block d** chidachi kilichotolewa na CBA Mkoa wa Dodoma. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
TAARIFA YA POLISI:
**PHQ/DOD/DOD/27229/2024**

## KUPOTELEWA NYARAKA YA UMILIKI KIWANJA

**EMMANUEL JOB KILONGE**
msimamizi wa Mirathi ya Job Ananiche Mwakilonge anatangaza kupotelewa na Nyaraka ya Umiliki **Kiwanja Namba 338 Kitalu "V"** kilichopo Ngokolo Manispaa ya Shinyanga
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Emmanuel kwa simu namba **0762-539333.**
TAARIFA YA POLISI:
**PHQ/SHI/SHI/4993/2024**

Josephat Peter Mushi
AFISA ARDHI
MANISPAA YA SHINYANGA

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**YOHANA EVARISTO MHANGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji yenye usjaili namba **MC 525 CVX.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/IRI/IRI/9187/2024**


**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,


PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**RAPHAEL AUGUSTINE LYARUU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **NP 0345/0125/2019** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **USAGALA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA : **PHQ/DAR/UBU/117182/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**RAHMA R KISUO** anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo kozi ya **BACHELOR OF LAWS** chenye namba ya usajili **TU/DARCO/LLB/016/237** kilichotolewa na **DAR ES SALAAM TUMAINI UNIVERSITY** mwaka 2019,yeyote atakaye kiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **PHQ/DAR/ILA/16290/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GASPER B.MFOY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1880-0177** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya **MBEZI HIGH** mwaka 2017,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **PHQ/DAR/UBU/129051/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**

**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI NA 13628 YA MWAKA 2024**
**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA**

**GEOFREY LUIWANA MREMA..................MAREHEMU**

**YUNISI FATAELI MOSHA...........................MUOMBAJI**

**TAARIFA KWA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 20 Mwezi Agosti, Mwaka 2024.

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 20 Mwezi JUNI Mwaka 2024.

DISTRICT COURT MWANGA

HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA
MWANGA

Hakimu Mkuu Mkazi Mfawidhi
Mwanga

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI NA BAJAJI

**ABRAHMAN ALLY NASSORO** anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki aina ya **SANLG** na **BAJAJI** aina ya **BOXER MC 895 BBG, T 221 CJJ, MC 121 BJS, MC 512 BPL, MC 222 BQH, MC 765 BQS, MC 251 BTD, MC 711 BVC, MC 785 CHF, MC 129 CXR.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/ILA/127976/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na. 24 /2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU ATHUMANI ALI KINGWELE WA CHAMWINO MJINI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA SHABANI ATHUMANI ALI KINGWELE**

**TANGAZO**
**( Kanuni ya 5(@) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 18 mwezi 07 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 26 mwezi 6 mwaka 2024

**Summons to appear (O.V, R.20(1) OF (Civil procedure code)**
**(substituted service)**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**

**AT DAR ES SALAAM**

**LAND CASE NO. 26059 OF 2024**

**PENUEL HILDER LAISER....................................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**TIB DEVELOPMENT BANK LIMITED & OTHERS ...................DEFENDANTS**

**TO:**
1. FIS AFRICAN STARCH DEVELOPMENT COMPANY LIMITED
2. ALLAN NALIGIA MAGOMA
3. IBRAHIM MICHAEL HAPE
4. MAZIKU BUNDARA
5. DEONATUS JULIUS MALEGESI
6. MARWA MTALA
7. EDWIN PANCRAS KATO
8. RONALD SYLVESTER RWEGASIRA

**WHEREAS:** The above named plaintiff has instituted the SUIT against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or authorized Agent on 18th day JULY, 2024 at 12:00 PM for HEARING of 1st PTC Before Hon, S. MWAIPOPO, judge to answer the said SUIT nad you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to reply insupport of your reply.
**TAKE NOTICE** that , in default of your appearance on that day, the said matter will be heard and determined in your absence.
Given under my hand and the seal of this court , this 20th day of JUNE, 2024

DEPUTY REGISTRAR

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**

**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NA 14471 YA MWAKA 2024**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU ROSEMARY MABEL KIGADYE**
**NA**
**RICHARD KIGELI KIGADYE ......................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**( kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 12 mwezi Saba, 2024. Saa 02:00 asubuhi . siku ambayo shauri hili limepangwa kusikilizwa mbele ya **Mhe. Jaji M. MNYUKWA.**
Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 21 Mwezi wa Juni, 2024.

NAIBU MSAJILI

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO. 14941 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late:**
**PETER ANTHONY KWEMBE**

**By 1: BERNADA PETER KWEMBE**
**2: ______________________**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 18TH day of JULY.2024

Dated at MOROGORO this 27TH day of JUNE.2024

MAHAKAMA YA WILAYA MOROGORO

RESIDENT MAGISTRATE

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
P.O.Box 660,Morogoro

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE DISTRICT DELEGATED COURT OF MOROGORO AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE;-**
**STELLA MKENDA MAGANGA..............DECEASED**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATIX BY;-**
**SAMWEL LEFI MAGANGA..........PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Made under rule 75 of the probate and Administration of Estate rules, CAP 352 R.E 2019)**

ALL person claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 04th day of July.2024.
Dated at Morogoro this .27th day of .June 2024.

Dated at Morogoro this .27th day of .June 2024
Senior Resident Magistrate
Morogoro District Court
MOROGORO

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
P.O.Box 660,Morogoro

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Kura ya maoni yaonyesha utata dhidi ya Joe Biden

**WASHINGTON,** Marekani

KURA mpya ya maoni inapendekeza kwamba baadhi ya wapiga kura wa chama cha Democratic wanazidi kuwa na wasiwasi kuhusu iwapo Rais Joe Biden (pichani chini) yuko sawa kiakili kuhudumu kama rais baada ya kuyumba kwenye mjadala wa Alhamisi.

Kura ya maoni ya 'CBS News/ YouGov' iliyotolewa juzi ilionyesha kuwa asilimia 72 ya wapiga kura waliojiandikisha wanaamini kuwa Rais Biden hana uwezo wa afya ya kiakili ya kuhudumu kama rais, ikiwa ni ongezeko kubwa kutoka asilimia 65 kwa waliokuwa na maoni kama hayo katika kura ya maoni ya awali.

Aidha, ilielezwa kuwa asilimia 49 ya wapiga kura walikuwa na maoni kama hayo kwa Rais wa zamani Donald Trump.

Ilielezwa kuwa jambo la kutia hofu kwa kampeni ya Rais Biden, asilimia 45 ya wanademokrasia waliojiandikisha ambao walijibu kura hiyo walisema wanaamini kuwa rais anapaswa kujiondoa na mgombea mwingine kuchukua nafasi yake.

Kiongozi huyo ana miaka 81 na Trump ana miaka 78. Na kwamba sauti ya kishindo ya Rais Biden na majibu ya kutatanisha, yalizua wasiwasi miongoni mwa baadhi ya Wanademokrasia kuhusu kugombea kwake na kuwaacha wengine wakitaka ajiondoe kwenye kinyang'anyiro cha kugombea urais.

Familia ya kiongozi huyo ilimtia moyo kusalia katika kinyang'anyiro hicho wakati wa ziara iliyopangwa kwa muda mrefu huko Camp David juzi, chanzo chenye kufahamu mazungumzo hayo kilithibitishwa na CBS News, mshirika wa BBC wa Marekani.

Mbunge wa Maryland, Jamie Raskin ambaye pia ni mshirika wa Democrat na White House, alielezea mahojiano yake kama wakati mgumu.

Raskin alisema kuna mazungumzo ya ukweli na mazito yanayofanyika katika kila ngazi ya chama chao, ingawa alisisitiza kuwa uamuzi wa mwisho unasalia kuwa wa Rais Biden.

"Licha ya uamuzi wowote utakaochukuliwa na Biden, chama chetu kitakuwa na umoja na pia kinamhitaji katikati mwa mijadala yetu katika kampeni," alisema. **BBC**



# Rais Ruto: Sina hatia vifo vya waandamanaji

**NAIROBI,** Kenya

RAIS wa Kenya William Ruto amesema kuwa hana hatia na vifo vya waandamanaji vilivyotokea mapema wiki iliyopita katika maandamano ya kuipinga serikali yake, yaliyosababisha taharuki kubwa siku chache zilizopita.

Ruto ametoa kauli hiyo wakati mamia ya watu wakikusanyika jana katika mji mkuu wa Nairobi kuwakumbuka watu waliouawa kwenye maandamano yaliyogeuka kuwa ya vurugu.

Katika mahojiano na kituo kimoja cha televisheni cha Kenya, Rais Ruto alisema idadi ya watu waliokufa ni 19, ikiwa ni takwimu za kwanza kutolewa na mamlaka. Huku akiahidi uchunguzi kamili kuhusiana na vifo vya waandamanaji.

Aidha, mashirika ya haki za binadamu yalitoa idadi ya vifo inayotofautiana na ya mamlaka yakisema kuwa watu wasiopungua 30 waliuawa katika maandamano yaliyochochewa na dhamira ya serikali ya kutaka kuongeza ushuru kupitia muswada wa fedha wa 2024.

Kutokana na machafuko yaliyojitokeza, Rais Ruto alibadili msimamo wake akisema kuwa atawasikiliza watu na hatosaini muswada huo kuwa sheria.

Maandamano hayo kwa kiasi kikubwa yalianza kwa amani na kugeuka kuwa ya vurugu siku ya Jumanne wiki iliyopita wakati wabunge walipoupitisha muswada huo kutokana na shinikizo kutoka shirika la fedha duniani (IMF).

Ilielezwa kuwa polisi walifyatulia risasi waandamanaji waliovamia majengo ya bunge na kuchoma moto. Akizungumzia vifo vya waandamanaji, Rais Ruto alisema kuwa "Ni kwa bahati mbaya. Kama demokrasia hayo hayapaswi kuwa sehemu ya mazungumzo yetu".

Aliongeza kuwa polisi walifanya kila waliloweza, na kama "kulikuwa na matumizi ya kupita kiasi, tunazo nyenzo za kuhakikisha tunashughulikia hilo. Ofisa yeyote muuaji ambaye alienda zaidi ya ilivyoainishwa kwenye sheria atachukuliwa hatua," alisema Rais Ruto.

Lakini ameonya kwamba wale waliovamia bunge pia watawajibishwa. "Wale waliovamia bunge na mahakama wamenaswa katika CCTV".

Akizungumzia uamuzi wa kuachana na muswada huo wa fedha dakika za mwisho, Ruto alisema kwamba hiyo inamaanisha wamerudi nyuma karibu miaka miwili na serikali itapaswa kukopa kwa uzito.

Aidha kiongozi huyo alikiri kwamba kama serikali walipaswa kutoa maelezo ya kina kuhusu muswada huo.

"Nikipewa nafasi ya kueleza watu wa Kenya muswada wa fedha ulikuwa unahusu nini na ungewafanyia nini, basi kila Mkenya angekubaliana nami," alisema Rais Ruto.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa juzi baadhi ya watu walikusanyika katika bustani ya Uhuru katikati mwa Nairobi, na kwamba baada ya kuimba na kuwasha mishumaa, walipeperusha bendera ya Kenya na kupita katika hospitali ambako baadhi ya majeruhi bado wanatibiwa. **DW**



Kiongozi wa Chama cha DA, John Steenhuisen, kushoto akisalimiana na Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa ambaye pia ni kiongozi wa Chama cha ANC. **PICHA: MTANDAO**

## Serikali mpya ya muungano Afrika Kusini

**CAPE TOWN,** Afrika Kusini

RAIS wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa ametangaza serikali mpya ya mseto, baada ya chama chake tawala cha 'African National Congress' (ANC) kupoteza wingi wa wabunge katika uchaguzi wa mwezi Mei, mwaka huu.

Baada ya kiongozi huyo kutangaza serikali hiyo jana, alisema serikali ya umoja wa kitaifa haijawahi kutokea katika historia ya demokrasia ya taifa hilo.

Ilielezwa kuwa chama cha ANC kitakuwa na nyadhifa 20 kati ya 32 za baraza la mawaziri, huku Chama cha Democratic Alliance (DA) ambacho ni chama kikuu cha upinzani kitashikilia nyadhifa sita na nyingine sita zitagawanywa kati ya vyama vidogo.

Aidha, inaelezwa kuwa kupungua kwa uungwaji mkono wa chama cha ANC katika uchaguzi kulionyesha kufadhaika kwa umma juu ya rekodi yake mbaya ya kutoa huduma za kimsingi na kukabiliana na ukosefu wa ajira, umaskini na ufisadi.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa ANC chini ya Nelson Mandela ilifanikisha lengo lake la kukomesha utawala wa wazungu walio wachache nchini Afrika Kusini mwaka 1994, na imekuwa ikitawala nchi hiyo hadi sasa.

Katika baraza jipya la mawaziri, ANC itashikilia wizara muhimu kama vile ulinzi, fedha na mambo ya nje. Huku chama cha DA kikishikilia nyadhifa kama wizara ya mambo ya ndani na ujenzi. Na kwamba kiongozi wa chama hicho John Steenhuisen ataongoza wizara ya kilimo.

Katika hotuba yake kwa njia ya televisheni siku ya juzi, Rais Ramaphosa alisema: "Serikali inayokuja itaweka kipaumbele ukuaji wa uchumi wa haraka na endelevu, na upatikanaji wa jamii yenye kuzingatia haki zaidi."

ANC ilikaribisha uamuzi huo kama hatua muhimu ya kusonga mbele, na ushahidi wa uthabiti wa demokrasia yetu nchini humo.

Wakati huo huo, DA ilisema "Ni fahari kukabiliana na changamoto hiyo na kuchukua nafasi yetu, kwa mara ya kwanza, kuingia katika serikali ya kitaifa. Pia tunaahidi utawala bora, kutovumilia kabisa rushwa na utungaji sera kwa vitendo."

Vile vile, licha ya makubaliano ya muungano wa baraza la mawaziri, malumbano makali ya kisiasa yameendelea kushuhudiwa kati ya vyama vya ANC na DA. **BBC**

HABARI MICHEZO

# COASTAL UNION KUWEKA KAMBI NCHINI COMORO

Na Shufaa Lyimo

TIMU ya Coastal Union ya Tanga imeanza mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA Kagame Cup), yatakayofanyika visiwani Zanzibar na jijini Dar es Salaam na baada ya hapo itahamishia kambi yao nchini Comoro, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe jana, kutoka jijini Tanga, Ofisa Habari wa timu hiyo, Abbas El Sabri, alisema wachezaji wote wameripoti kambini isipokuwa wale wa kimataifa ambao wataanza kuripoti kuanzia leo.

**"Leo (jana) jioni tumeanza mazoezi rasmi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Cecafa huku tukiwa tunasubiri ratiba ili tujue tumepangwa kuanzia Dar es Salaam au Zanzibar," alisema El Sabri.**

Alisema mashindano hayo wanayachukulia kama maandalizi ya kujiandaa na mashindano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, pamoja na Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Ofisa habari huyo alisema wiki mbili watazitumia kwenye Kambi ya CECAFA na kudai wiki mbili zitakazobaki watakwenda kuweka kambi nchini Comoro ikiwa ni maandalizi ya msimu ujao.


Alisema malengo yao ni kufanya vema kwenye mashindano hayo ambayo yatawasaidia kuangalia uwezo wa kila mchezaji ikiwamo wale wapya waliowasajili msimu huu.

Aliwataka mashabiki wao kuendelee kuwapa ushirikiano kama walivyofanya msimu uliopita ili watimize malengo yao waliyojiwekea.

Coastal Union na Simba zitaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika wakati Yanga na Azam FC zikibeba jukumu la kuiwakilsha Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa.

Miamba hiyo ya Tanga, imepata nafasi hiyo baada ya kumaliza nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara msimu uliomalizika, huku Simba ikimaliza ya tatu na Yanga ikiwa kinara wa ligi hiyo wakati Azam ikishika nafasi pili.

WANIA...



Beki wa kulia wa Mexico, Jorge Sanchez (kushoto), akiwania kumiliki mpira dhidi ya winga wa Ecuador, Jeremy Sarmiento, wakati timu hizo zikitoka suluhu kwenye mechi ya michuano ya Copa America, iliyopigwa Marekani jana. Matokeo hayo yanaifanya Ecuador kufuzu hatua inayofuata huku Mexico ikiaga mashindano. **PICHA: MTANDAO**

# *Pamba kuibomoa Tabora United*

Na Adam Fungamwango

KATIKA kujiimarisha kabla ya kuanza kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza baada ya miaka 23, Klabu ya Pamba ipo kwenye mazungumzo na straika Eric Okutu wa Tabora United.

Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema viongozi wa klabu hiyo tayari wameshamshawishi raia huyo wa Ghana aliyesajiliwa na Tabora United kutoka Klabu ya Hearts of Lions FC ya Ghana kiasi kwamba ameanza kuomba kuondoka ndani ya kikosi hicho.

"Tunahitaji straika mzuri ambaye anaweza kutupa walau mabao 10 tu kwa msimu, tumeona kuwa Okutu anaweza kufanya hivyo kwa sababu tumesajili viungo wazuri wa kuweza kumlisha," alisema mtoa taarifa huyo.

Imeelezwa kuwa Kocha Mkuu mpya wa klabu hiyo, Goran Kopunovic, ndiye aliyeshauri kuletewa straika huyo kwani alifanya naye kazi akiwa na Tabora United msimu uliopita.

Mghana huyo akicheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza alipachika mabao saba, hivyo kuwatoa udenda viongozi wa Pamba na kocha wao.

Wakati huo huo, klabu hiyo imemtangaza, Salvatory Edward kuwa kocha msaidizi wa kikosi hicho.

Nahodha huyo wa zamani wa Yanga anakwenda kumsaidia Goran kusuka kikosi hicho ambacho kimepanda Ligi Kuu msimu huu baada ya kuteremka 2001.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo, imemtangaza pia, Kakooza Rogers raia wa Uganda kuwa kocha wa viungo wa kikosi hicho.

Mganda huyo atakuwa na kazi ya kuwafua wachezaji hao ili wawe na fiziki na pumzi, kabla ya ligi kuanza na wakati ikiendelea.

## Serikali yataka mikoa nane kufufua gofu

Na Godfrey Mushi, ARUSHA

MIKOA yote yenye viwanja vya gofu nchini, vitaanza kutumika rasmi kuanzia Julai 20, mwaka huu, kwa ajili ya kuandaa vijana watakaounda timu ya taifa ya mchezo huo, amesema Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro.

Akizungumza jijini Arusha jana, wakati akifunga michuano ya Gofu ya NCBA Series 2024, alisema wizara hiyo inaanza kutekeleza agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa la kutaka kuanzia mwaka ujao, mchezo wa huo kuanza kuchezwa katika mashindano ya Umoja wa Michezo ya Shule za Sekondari Tanzania (UMISSETA).

"Tutaanza kuvitumia kuanzia Julai 20, mwaka huu, kwa kuaanza kutoa mafunzo kwa walimu na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari. Kwa hiyo Mkoa wa Kilimanjaro, Arusha, Dodoma, Iringa, Morogoro, Dar es Salaam, Zanzibar na uwanja mpya wa Fort Ikoma, kule Serengeti (Mara), shule ambazo ziko jirani nao tutatoa mafunzo hayo.

"Tunaamini shule hizo mwakani, zitaweza kushindana na tutatengeneza timu nzuri za vijana za taifa. Kwa sababu lengo letu sasa ni kuwa na timu kubwa ya vijana ya taifa ili baada ya miaka mitatu, mitano; vijana hawa waweze kushindana kimataifa na tufanye vizuri zaidi.

"Gofu si mchezo wa matajiri, ukiangalia hapa hata wanaocheza ni watu wa rika zote. Labda ni kwa sababu matajiri wote wanapenda kucheza gofu, lakini haizuii watu wa kawaida nao kucheza," alisema Dk. Ndumbaro

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mchezo wa Gofu Tanzania, Gilman Kasiga, akizungumza katika viwanja vya Gymkana Arusha, alisema mashindano ya NCBA Gofu Service yanayoendeshwa Afrika Mashariki yote, yanalenga kuinua mchezo huo na kukuza vipaji vya wachezaji wadogo.

"Mshindi wa leo ataingia fainali ya NCBA Series itakayofanyika Nairobi, Kenya, Novemba mwaka huu. Tunafurahi sana kwamba NCBA wamekuwa wadau wetu muhimu sana wa Gofu Tanzania.

"Lengo letu ni kuendeleza mchezo huu, kwa maana hiyo kupata 'partners' (washirika) kama NCBA ambao tunashirikiana nao katika mchezo huu, sisi tumefarijika sana,"alisema.

## ZISIKUPITE

### CALAFIORI ANYATIWA

LIVERPOOL, Arsenal, Chelsea na West Ham zote zinavutiwa na beki wa Italia, Riccardo Calafiori mwenye umri wa miaka 22, lakini watalazimika kulipa zaidi ya pauni milioni 40 ili kumnunua kutoka Bologna. ***(Express)***

### WILLIAMS HAJASHAWISHI

BAADHI ya wakurugenzi wa Barcelona bado hawajashawishika kuhusu ubora wa kumsajili winga nyota wa Hispania kwenye Euro 2024, Nico Williams mwenye umri wa miaka 21, kutoka Athletic Bilbao. ***(Sport)***

### HALL HUYOOO CHELSEA

KLABU ya Brighton imeachwa mdomo wazi baada ya Chelsea kukubali dili la kumsajili kiungo, Kiernan Dewsbury-Hall mwenye umri wa miaka 25, kutoka Leicester ingawa mchezaji huyo alikuwa amefanyiwa uchunguzi wa kimatibabu na Seagulls na ada ilikubaliwa kati ya klabu hizo mbili. ***(Telegraph)***

### ARAUJO HANUNULIWI

KLABU ya Manchester United haina nia ya kutafuta dili la kumnunua mlinzi wa Barcelona, Ronald Araujo licha ya nia ya muda mrefu ya kumnunua mchezaji huyo wa Kimataifa wa Uruguay mwenye umri wa miaka 25. ***(Football Transfers)***

### GOLDING ANUKIA LEICESTER

KLABU ya Leicester City inakaribia kufikia makubaliano ya kumnunua kiungo wa kati Michael Golding mwenye umri wa miaka 18, kutoka Chelsea. ***(The Athletic)***

### KUDUS KUIACHA WEST HAM

MCHEZAJI wa Ghana, Mohammed Kudus mwenye umri wa miaka 23, amekuwa akihusishwa na kutaka kuondoka West Ham, lakini klabu hiyo bado haijapokea ofa ya kiungo huyo mshambuliaji. ***(Sky Germany)***

### OSIMHEN AWEKWA SOKONI

KLABU ya Napoli itazingatia ofa ya kiwango cha euro milioni 100 kwa mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 25, na mshambuliaji wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku anayetarajiwa kuchukua nafasi yake. ***(Calciomercato)***

### VLACHODIMOS ATAKIWA

NEWCASTLE United inajaribu kufanya mazungumzo ya kumsajili mlinda mlango wa Nottingham Forest na Ugiriki, Odysseas Vlachodimos mwenye umri wa miaka 30, kama sehemu ya uhamisho wa kiungo wa kati wa Scotland, Elliot Anderson mwenye umri wa miaka 21, kwenda City Ground. ***(Daily Mail)***

### NEWCASTLE KUMZUIA ISAK

KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe, ameweka wazi katika mazungumzo na bodi ya klabu hiyo kwamba hawatakiwi kumuuza mshambuliaji wa Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 24, msimu huu huku kukiwa na nia kutoka kwa Chelsea. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RODRIGO NI KOMPYUTA YA HISPANIA - KOCHA

**COLOGNE,** Ujerumani

KOCHA wa Hispania, Luis de la Fuente, amesifu jukumu la Rodri wakati timu yake ikitoka nyuma na kuifunga Georgia mabao 4-1 na kutinga robo fainali ya Euro 2024, hivyo sasa itakutana na wenyeji, Ujerumani mjini Stuttgart Ijumaa wiki hii.

**Rodri wa Manchester City alifunga bao la kusawazisha baada ya bao la kujifunga la Robin Le Normand na kuipa Georgia uongozi wa kushtukiza katika kipindi cha kwanza.**

kutokana na kiwango cha juu alichokionesha, Rodri alitangazwa kuwa mchezaji bora wa mechi huku Fabian Ruiz, Nico Williams na Dani Olmo kila mmoja akifunga.

●●● Anaweza kufanya kila kitu wakati wote kikamilifu, ni msaada mkubwa kwa...

"Ni kawaida kwamba baada ya bao la kujifunga, kulikuwa na dakika za wasiwasi," aliseema De la Fuente katika mkutano wake na waandishi wa habari.

"Lakini tuliweza kushindana nyuma na wachezaji walisoma mchezo kwa ustadi. Tulikuwa watulivu wakati wa mapumziko, hakukuwa na wasiwasi na wachezaji walijua kinachohitajika.

"Na kisha tuna Rodri, ambaye ni kompyuta ambaye hufanya kila kitu. Alisimamia hisia zote na wakati wote kikamilifu, ambayo ni msaada mkubwa kwa kila mtu," alisema.

Hispania walisajili mikwaju 35 kwenye goli mwishoni, idadi yao ya juu zaidi katika michuano mikubwa kuwahi kurekodiwa tangu mwaka 1980, huku De la Fuente akihisi walipaswa kufunga mabao mengi zaidi.

"Matokeo hayakuonesha mchezo kwa sababu tungeweza kushinda 8-1 au 9-1," aliongeza.

"Lakini siku zote ni ngumu katika hatua hii ya mashindano na lazima uteseke wakati hauchukui nafasi zako."

HABARI MICHEZO

# KEPA KWENYE RADA ZA REAL MADRID



**MADRID,** Hispani

REAL Madrid iko tayari kumnunua tena mlinda mlango Kepa Arrizabalaga iwapo Andriy Lunin ataondoka, kwa mujibu wa ripoti kutoka Hispania.

Kepa alijiunga na 'Los Blancos' hao kwa mkopo mnamo Agosti 2023, akiingia baada ya Thibaut Courtois kuumia.

Madrid ilikataa uhamisho wa kudumu kwa Kepa, ambaye aliangushwa kwenye chaguo la tatu wakati Courtois aliporejea na kurudishwa Chelsea.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Marca, Madrid wanaweza kufikiria upya msimamo wao kuhusu Kepa, ambaye anaweza kurejeshwa klabuni hapo ikiwa Lunin ataamua kuondoka.

Mkataba wa sasa wa Lunin umesalia miezi 12 tu kumalizika na nyongeza bado haijatiwa saini, ingawa mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ukraine pia hajaomba kuondoka katika klabu hiyo.

Akiwa ameonesha kiwango kizuri katika kipindi chake kama nyota, Lunin amevutia watu wengi kutoka mahali pengine, na ikiwa ataamua kuondoka inaripotiwa kwamba Madrid inaweza kutafuta kumrudisha Kepa.

Chelsea wanataka kumuuza Kepa kabisa msimu huu wa majira ya joto huku akiingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake.

Kepa pia ana nia ya kurejea Madrid, hivyo mazungumzo yanaweza yasiwe na changamoto kwa yeyote anayehusika, lakini mustakabali wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, bado umefungwa na Lunin kwa sasa.

## *Southgate na siri England kutinga robo fainali Euro*

**DUSSELDORF,** Ujerumani

KOCHA Gareth Southgate anaamini kuwa video iliyooneshwa kwa kikosi cha England katika kampeni yao ya kushinda Kombe la Dunia la mwaka 1966, ilisaidia kushinda mabao 2-1 Jumapili dhidi ya Slovakia kwenye hatua ya 16 bora ya michuano ya Euro 2024.

'Simba Watatu' hao walitoka nyuma baada ya bao la ufunguzi la Ivan Schranz dakika ya 25, ambapo Jude Bellingham aliisawazisha dakika ya 95 na kulazimisha muda wa nyongeza.

Harry Kane kisha akafunga bao la ushindi baada ya sekunde 60 ndani ya muda wa ziada wa dakika 30 na kutinga robo fainali ambapo sasa watacheza na Uswisi mjini Dusseldorf Jumamosi.

Baada ya mchezo huo, ambao Southgate alitumia wachezaji watano wa akiba, alielezea video iliyooneshwa kwa wachezaji wakiwa St George's Park kabla ya mchuano huo, ambayo ilieleza umuhimu wa kila mshiriki wa kikosi hicho kilichoshinda taji kuu pekee la England.

"Tuliwaonesha wachezaji mada kuhusu mwaka 1966 na jinsi Geoff Hurst ambaye alifunga 'hat-trick' (mabao matatu katika mechi moja) kwenye fainali ya England ilipoishinda Ujerumani Magharibi 4-2 hakucheza hadi robo fainali na njia ngumu ambayo timu ilikuwa nayo," alisema Southgate.


"Wakati wote, wachezaji ambao wameingia kwenye michezo wamekuwa na mchango mkubwa. Wamekuwa tayari, wamefanya mazoezi ya kutosha na wachezaji wote walioingia walicheza majukumu muhimu katika kuunda mabao.

"Conor Gallagher akijirusha kusimamisha mpira kuingia eneo letu. Hiyo ndiyo roho waliyonayo na ndiyo imetufanya tuvuke mstari.

"Tulitaka tu kuangazia kwamba mashindano yanakupeleka katika maeneo ya ajabu, njia ngumu. Timu haikuwa ikiruka kila mara. Timu nina uhakika ingekosolewa mwanzoni kwa hivyo ulikuwa ni mtazamo kidogo tu.

"Tulitaka kuangazia thamani ya kikosi, ukweli kwamba baadhi ya wachezaji ambao unadhani watakuwa kama Jimmy Greaves wanaishia kucheza nafasi tofauti.

"Ni moja ya mambo ambayo tumefanya ili kutambua thamani ya kundi. Daima tunarejelea nyakati hizi kwa sababu hiyo ndiyo sehemu ya kuunda timu itakayoshinda mashindano. Tuna safari ndefu."



## United wateta na de Ligt

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imefanya mazungumzo na wawakilishi wa beki wa kati wa Bayern Munich, Matthijs de Ligt, kwa mujibu wa ripoti.

'Mashetani Wekundu' hao wanatafuta kuimarisha safu ya ulinzi ya Erik ten Hag baada ya kuondoka kwa Raphael Varane kwa uhamisho huru, na wamekuwa wakihusishwa sana na Jarrad Branthwaite wa Everton na Jean-Clair Todibo wa Nice.



Jina la De Ligt pia limekuwa likijadiliwa mara kwa mara katika safu za uvumi huku kukiwa na mustakabali usio na uhakika kule Bayern.

Mholanzi huyo alikuwa hana nafasi chini ya kocha wa zamani, Thomas Tuchel na inasemekana kutoridhishwa na msimamo wake huko Bavaria.

Vyanzo vingi vya habari vimeripoti kwamba United wamefanya mazungumzo na kambi ya De Ligt juu ya kuhamia Old Trafford, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, anasemekana kuvutiwa na uhamisho huo.

De Ligt amehamishwa mara mbili kwa kiasi cha fedha kisicho cha kawaida baada ya kuhitimu kutoka akademia maarufu ya Ajax.

Juventus walimnasa kwa mkataba wa miaka mitano mwaka 2019, wakiwalipa wababe hao wa Uholanzi karibu euro milioni 75, na miaka mitatu baadaye aliigharimu Bayern hadi ya euro milioni 77.

# AZAM YAMPIGA BEI KIPRE JUNIOR MC ALGER, FEI TOTO BADO YUPO

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam imethibitisha kuwa imefikia makubaliano na MC Alger ya Algeria kuwauzia mchezaji wao, Kipre Junior, raia wa Ivory Coast kwa kiasi cha Dola 300,000 za Kimarekani sawa na Sh. milioni 824 za Tanzania.

**Klabu hiyo imesema hayo baada ya kuzuka tetesi hivi karibuni kuwa mchezaji huyo anayecheza nafasi ya winga zote mbili na kiungo mshambuliaji kutakiwa na klabu hiyo.**

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Azam, Thabit Zacharia maarufu Zaka Zakazi, amesema jana kuwa mazungumzo ya pande zote mbili yamekamilika na kilichobaki sasa ni kuandikishiana mikataba.

"Ni kweli MC Alger wametuma ofa yakafanyika mazungumzo marefu baina yetu na wao na kufikia muafaka, ninavyokwambia ni kwamba muafaka umefikiwa, kilichobakia ni taratibu zingine kwamba huyu bwana anaondoka, klabu imeshakubali ila kilichobaki ni kuandikishiana mikataba ndiyo hatua zinazofuata," alisema Zaka Zakazi.

Hata hivyo, alisema haikuwa nia ya klabu kumuuza, ila klabu hiyo ya Algeria imekubali kutoa kiasi hicho kilichowekwa kwenye mkataba baina ya Azam na mchezaji huyo kama ikitokea timu inayomtaka.

"Tunamuuza pesa nyingi sana, sisi tukiwasajili wachezaji kwenye mikataba tunaweka kipengele cha pesa ambayo anaweza kuuzwa, huyu tuliweka dola 300,000 za Kimarekani na jamaa wameweka huo mzigo, hapo huwezi kusema chochote, labda mchezaji tu akatae," alisema.

Kipre alikuwa amebakisha mwaka mmoja na Klabu ya Azam, akisajiliwa misimu miwili iliyopita kutoka Sol FC ya Ivory Coast.

Msimu uliomalizika amehusika na mabao 18, akifunga tisa na kutoa pasi za mwisho tisa, na kuwa kinara wa 'asisti' kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2023/24.

Aidha, Zaka alikiri Klabu ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini kutaka kumtwaa kiungo mshambuliaji wao tegemeo, Feisal Salum, lakini hawakufikia kile kiwango walichokiweka cha kuvunja mkataba.

"Nayo ni kweli, ila niwakumbushe watu kuwa wachezaji wetu hawapo sokoni, hata Kipre hatukuwa tunamuuza ila ukiwataka fikia malipo yaliyoandikwa kwenye mkataba, yaani kile kipengele cha pesa tulichoweka, MC Alger wamefikia, ila Mamelodi Sundowns wao hawakufikia hicho kiwango kwa hiyo Fei Toto bado yupo," alisema Zaka.




Winga wa Hispania, Lamine Yamal (kushoto), akijaribu kufunga lakini kipa wa Georgia, Giorgi Mamardashvili, akawa makini kuokoa hatari hiyo katika mechi ya Euro 2024 iliyopigwa Ujerumani juzi. Hispania ilishinda mabao 4-1 na kutinga hatua ya robo fainali ambapo sasa itakutana na wenyeji, Ujerumani. **PICHA: MTANDAO**

## Rais ZFF asifu Z'bar kusheheni vipaji vya soka

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Dk. Suleiman Mahmoud Jabir, amesema Zanzibar imejaliwa vipaji vingi vya soka ambavyo huhitaji kuvitafuta bali kinachohitajika ni kuvilea na kuviendeleza.

Hayo aliyaeleza alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika Uwanja wa Mao Zedong B, baada ya kumaliza ufunguzi wa mashindano ya akademi za vijana yanayoendelea visiwani hapa.

Alisema ni jambo la kufurahisha na kuona kuwa wana waalimu ambao wamewakusanya vijana hao kwa ajili ya kuvitunza na kuvilea vipaji hivyo.

"Lakini pia nishukuru kuona mashindano ni ya akademi lakini pia na umri uliopo, hivyo unaweza kuona kwamba kuna vipaji vinatafutwa, vinalelewa na kuendelezwa," alisema.

Sambamba na hayo alichukuwa fursa hiyo kutoa shukrani zake kwa wazazi wa watoto hao kwa kuona umuhimu wa uwapo wa mashindano hayo na kuhakikisha yanafanyika.

Katika mashindano hayo ambayo yameandaliwa na Akademi ya YFDA, yanashirikisha watoto chini ya miaka 10, 14, 16 na 20 na hii ni mara ya pili kufanyika kwake na mara ya mwisho ilifanyika mwaka jana.

Mashindano ya Zanzibar Akademi 2024 yanashirikisha akademi 11 zilizotoa timu 20, zikiwamo Akademi ya Small Simba, Mamboul, New Boys, All Star, Korosini City, JKU, Mkokotoni, Muyuni, Beitras na wenyeji YFDA.

## *Mrithi wa Chama Simba huyu*

INATOKA UKURASA 24

watakapoanza kutangaza mmoja baada ya mwingine.

Amekiri kuwa baadhi ya wachezaji wataingia wiki hii, lakini tayari kuna wachezaji saba wametua kwa ajili ya kumalizana na uongozi.

"Tuna wachezaji wapya saba wa kigeni wapo hapa hapa Tanzania kwa ajili ya usajili, bahati nzuri si watu wengi wanaowafahamu, lakini pia wapo chini ya ulinzi mkali, napenda kuwaambia wanachama na mashabiki wa Simba wasione kimya wakadhani hakuna kinachofanyika.

"Wakati haya majembe saba yapo Dar, baadhi ya viongozi wetu wamegawana majukumu, mwingine Zambia, yupo aliyekwenda Ivory Coast, kuna anayesafiri kwenda Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, mmoja Maylasia, kote huko kwenda kumalizana na wachezaji," alisema Ahmed.

Alisema kwa mara ya kwanza baada ya misimu mingi Simba itakuwa na wachezaji wengi wapya kwenye kikosi chake na hii inafanywa makusudi na uongozi ili kutengeneza timu mpya itakayorudisha heshima ya klabu hiyo.

"Tunafanya ukarabati mkubwa, timu hii lazima tuijenge upya, watu wamechoka, wanataka furaha, wanataka makombe, hawataki kuendelea kuyaona ya zamani, wanataka kuyaona mapya, huwezi kuyapata kama hujatengeneza timu bora," alibainisha Meneja Habari huyo.

## Nyota kumtesa Gamondi

INATOKA UKURASA 24

Baadhi ya wachezaji waliochezea timu hizo kwa nyakati tofauti katika kipindi cha hivi karibuni ni Ramadhan Waso, Mike Barasa, Emmanuel Okwi, Amissi Tambwe, Hamis Kiiza, Haruna Niyonzima, Benard Morrison na Saido Ntibazonkiza.

Inaelezwa Chama aliugawa uongozi wa Simba katika kufanya maamuzi ya kumuongezea mkataba au kuachana naye ili kusajili mchezaji mwingine.

Mtoa taarifa wetu kutoka ndani ya klabu hiyo ya Simba anasema uongozi wa klabu hiyo uligawanyika ambapo wapo ambao walitaka nyota huyo asiongezewe mkataba kwa kuwa kiwango chake kimeisha na amekuwa msumbufu, lakini wapo waliotaka nyota huyo kuongezewa mkataba.

# Michezo

Jumanne Julai 2, 2024

Nipashe




Kepa kwenye rada za Madrid

UKURASA 22

TAMBUKA!...



Kiungo wa England, Jude Bellingham 'akitambuka' na kuifungia timu yake bao la kusawazisha wakati wakishinda mabao 2-1 dhidi ya Slovakia, katika mechi ya hatua ya 16-bora ya michuano ya Euro 2024 iliyopigwa Ujerumani juzi. Anayeshuhudia huku akijiandaa kwa lolote ni mfungaji wa bao la pili, Harry Kane. **PICHA: MTANDAO**

# MRITHI WA CHAMA SIMBA HUYU HAPA

**Na Adam Fungamwango**

## Ni MVP wa Ligi Kuu Ivory Coast, kiboko wa kutupia na mpishi wa mabao, majembe saba yawasili...

WAKATI Yanga ikitangaza rasmi kumsajili Mzambia Clatous Chama, baada ya kumaliza mkataba na klabu yake ya zamani, kiungo mshambuliaji anayetajwa kuja kuchukua nafasi yake Simba, Jean Charles Ahoua (pichani), anatarajiwa kutua wiki hii nchini kukamilisha usajili.

**Habari zilizopatikana ndani ya Klabu ya Simba, na vyanzo mbalimbali vya habari za mchezo Afrika Magharibi, zinasema, Ahoua atasafiri kutoka nchini kwao Ivory Coast kuja nchini kukamilisha usajili wake ambapo kila kitu kimekamilika, kilichobaki ni yeye kutua na kusaini mkataba wa miaka mitatu na kisha kutambulishwa.**

Ahoua ndiye mchezaji bora (MVP) kwenye Ligi Kuu nchini Ivory Coast, akiichezea Klabu ya Stella Club d'Adjame ya nchini humo, ambapo amepachika mabao 12 na 'asisti' tisa, hivyo kuhusika katika jumla ya mabao 21 msimu wa 2023/24.

"Huyu ndiye mrithi sahihi wa Chama, anawasili wiki hii, anacheza kiungo mshambuliaji, namba 10, ni mchezaji bora wa msimu wa 2023/24 nchini Ivory Coast, amehusika katika mabao 21, amefunga 12 na asisti tisa, sasa nikwambie tu huyu mchezaji amesajiliwa rasmi kwenda kuchukua mikoba ya Chama, huyu ndiye atakayeuzika ufalme wake.

"Viongozi wameachana na Chama kwa sababu kwanza



umri umekwenda halafu amekuwa msumbufu, na kwa kiasi kikubwa kwa kipindi cha karibuni nidhamu yake haikuwa nzuri," alisema mtoa taarifa wetu ndani ya klabu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri miaka 22, alizaliwa Februari 10, 2002 nchini humo, na alianza soka la ushindani, mwaka 2020 alipocheza kwenye Klabu ya LYS Sassandra na mwaka huo huo, akahamia Sewe FC, ambayo alikipiga nayo hadi 2022, alipojiunga na Stella Club d'Adjame kabla ya kuwavutia mabosi wa Simba ambao baadhi yao walisafiri mpaka nchini humo kutaka huduma yake.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, amesema kwa sasa wanaendelea na usajili na mpaka watakapomaliza ndipo

INAENDELEA UKURASA 23

# Nyota Yanga mtihani kwa Gamondi

**Na Faustine Feliciane**

MABINGWA wa soka Tanzania Bara, Yanga jana ilitangaza kumsajili mchezaji wa zamani wa Simba, Clatous Chama, ambaye ataichezea timu hiyo msimu ujao kwenye Ligi Kuu na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Usajili huo unatajwa kuwa mtihani kwa kocha Miguel Gamondi katika kuamua nani aanze kwenye kikosi hicho ambacho sasa kitakuwa na wachezaji watatu wenye uwezo wa kucheza nafasi ya kiungo wa kati na mshambuliaji namba 10.

Kabla ya kusajiliwa kwa Chama, Gamondi amekuwa na nyota watatu wenye uwezo mkubwa wa kucheza namba hizo, ambao ni Max Nzengeli, Aziz Ki na Pacome Zouzoua ambao wamekuwa wakimpa matokeo chanya kwenye michezo mbalimbali.

Mmoja wa viongozi wa klabu hiyo, aliliambia Nipashe jana kuwa uongozi umekamilisha usajili wa Chama na sasa kazi imebaki kwa Gamondi kukuna kichwa kuamua nani atakuwa anaanza kati ya nyota hao.

"Tunaamini ni usajili wenye tija, kuna kitu kinaenda kuongezeka kwenye kikosi, hapa kazi ipo kwa kocha na ni mtihani kwake katika kuamua nani aanze na kwenye nafasi gani, tunataka Yanga iwe bora zaidi ya msimu uliopita," alisema kiongozi huyo ambaye hakutaka jina lake liandikwe.

Usajili huo wa Chama ndani ya Yanga sasa utamfanya kocha Gamondi kuwa na machaguo mengi kwenye nafasi ya mshambuliaji namba 10 na kiungo wa kati ingawa Mzambia huyo pia ana uwezo wa kucheza kama mshambuliaji anayetokea pembeni kama ilivyo kwa Pacome.

Chama amejiunga na Yanga baada ya tetesi za muda mrefu, Mzambia huyo alimaliza mkataba wake wa kuichezea Simba Juni 30, mwaka huu na kuwa huru kujiunga na timu yoyote.

Mzambia huyo amesaini mkataba wa mwaka mmoja huku ikitajwa kupewa dau kubwa la usajili na anakuwa mchezaji mwingine katika kundi la wachezaji wachache wa kimataifa kuzichezea Klabu za Simba na Yanga.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >